SportPesa
TZS.1,255,316,060
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 4

## WAKILI maarufu atangaza mbinu kuiendeleza TLS


Ukurasa 13
Hivi kweli Uviko-19 unaishi kwa adabu?
BUFE
IJUMAA MEI 13, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
TARI RASMI YAGONGA HODI... Kung'ara kwa walima tangawizi kitaifa Same na magonjwa 'kuwavuta shati'
Ukurasa 14
Waliokabiliwa na adha zote za umasikini na makazi, wazawadiwa nyumba mpya
• Makazi yao na walivyoishi...Mungu anajua!
• Mjane alipoonyeshwa jengo lake, alianguka
Na Mary Mosha, MOSHI

UKURASA 11

# Nipashe

Ijumaa Mei 13, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580944

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Dk. Bagonza aibuka sakata kina Mdee

UKURASA 2



Askofu Benson Bagonza.

Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe

Mwonekano wa viti upande wanaokaa wabunge wa kambi ya upinzani Bungeni, vikiwa wazi kutokana na wabunge 19 wa viti maalumu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kutoonekana kwenye kikao cha 21 cha mkutano wa saba wa Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wanawake watano wauawa, wanyofolewa sehemu za siri

UKURASA 3

## YALIYOMO

**UKURASA WA 2**

### WATUHUMIWA UHALIFU WAZIDI KUKAMATWA

OPERESHI ya kuwasaka vijana wanaofanya uhalifu mitaani, maarufu 'panya road', mkoani Dar es Salaam imewakamata watuhumiwa...

**UKURASA WA 4**

### SERIKALI NA WADAU WA UTALII KUTETA TIJA FILAMU ROYAL TOUR

SERIKALI inakutana na wadau wa utalii, zikiwamo hoteli zilizosimama kutoa huduma, ili kuimarisha sekta hiyo inayotarajiwa kupokea...

**UKURASA WA 5**

### WANAFUNZI 153,220 WACHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO, UFUNDI

WANAFUNZI 153,219 wakiwamo wasichana 67,541 na wavulana 85,678 sawa na asilimia 91.8 ya wenye sifa, wamechaguliwa kujiunga...

## Waziri Aweso aanika mipango kumaliza kero ya maji nchini

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA SC: MALENGO YA UBINGWA YAKO PALEPALE UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimwapisha Shekhe Hassan Othman Ngwali kuwa Kadhi Mkuu wa Zanzibar, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Bagonza aibuka sakata kina Mdee

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimesema kimeshaandaa barua ya kumpelekea Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson, kuhusu uamuzi uliochukuliwa na kamati kuu ya chama hicho wa kuwavua uanachama waliokuwa wanachama wao 19, akiwamo aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake (BAWACHA), Halima Mdee.

Wakati chama hicho kikiendelea na mchakato huo, Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe, Dk. Benson Bagonza, amesema uamuzi uliofanywa na chama hicho unapaswa kupewa heshima huku akiitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Bunge, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, serikali na vyama vya siasa kujifunza kutokana na sakata hilo.

Uamuzi wa kuwavua uanachama ulikuja baada ya kwenda kuapishwa na kuwa wabunge wa viti maalumu bila kupata baraka ya chama hicho jambo lililotafsiriwa kama usaliti. Usiku wa kuamkia jana, Baraza Kuu la chama hicho lilibariki uamuzi wa kuwafuta uanachama.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alisema barua hiyo ipo njiani na muda wowote kuanzia sasa itafika mezani kwa Spika wa Bunge.

**HATIMA RUZUKU**

Kuhusu ruzuku, Mnyika alisema hawezi kulizungumzia kwa sasa kwa sababu kamati kuu ya chama ndiyo yenye wajibu wa kukaa kikao na kujadili kama watachukua ruzuku au la.

"Kikao cha kamati kuu kina wajibu wa kujadili suala la ruzuku na mpaka sasa bado hawajakaa kikao, kwa hiyo siwezi kulizungumzia mpaka pale kamati hiyo itakapokaa," alisema.

CHADEMA kilitangaza kususia ruzuku na vyote vinavyopatikana kupitia uchaguzi mkuu uliopita, ikiwamo ubunge wa viti maalum na kueleza kuwa hakitambui matokeo ya uchaguzi huo na mchakato wake.

Kufuatia msimamo huo, CHADEMA iligoma kupeleka kwa msajili wa vyama, jina la akaunti ya Baraza la Wadhamini, ili kuingiziwa fedha za ruzuku.

**BAGONZA NA FUNZO**

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe, Dk. Benson Bagonza, alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia uamuzi wa Baraza Kuu CHADEMA, alisema uheshimiwe kama ambavyo wabunge hao walivyokuwa na imani nao kuwa watatendea haki.

"Wale wabunge 19 nafikiri walikuwa na imani na baraza kuu na ndiyo maana wakaandika rufani yao, huwezi kutuma rufani kwa mtu usiyeamini kuwa atakutendea haki. Kwa hiyo, waliandika rufani zao, baraza limeitisha, limefanya uamuzi, nadhani uamuzi wa baraza uheshimiwe na wote," alisema.

Askofu Bagonza pia alisema kuwa kuna kitu cha kujifunza kama taifa kupitia sakata hilo huku, swali kuu likiwa ni 'kitu gani kiliwapeleka wabunge hao bungeni ilhali chama chao hakikuridhia?'

"Liwe fundisho kwa Tume ya Uchaguzi, Msajili wa Vyama, uongozi wa Bunge wenyewe, serikali, vyama vya siasa, kila mtu ana la kujifunza katika hili," alisema.

Alisema kufuatia uamuzi huo CHADEMA imeonyesha ukomavu wa kisiasa kwa sababu imefanya jambo ambalo vyama vingine vya kisiasa havikufanya, ikiwamo kushirikisha wadau wa siasa katika mchakato wa kufanya uamuzi huo.

"Wamefanya kitu ambacho hakikufanywa na wengi, tumesikia vyama vikifukuza wanachama wake ikiwamo chama tawala (CCM), hatujawahi kusikia mpaka na msajili anashiriki kwenye baraza anaona jinsi mambo yalivyokwenda, naweza kusema wamekomaa," alisema.

Akiongelea suala la katiba mpya askofu huyo alisema kuwa wakati wa kupata katiba hiyo ulishafika na kupita tangu zamani hivyo kinachohitajika ni mchakato wa upatikanaji wake.

Mchambuzi wa siasa nchini, Gwandumi Mwakatobe, alisema anawapongeza CHADEMA kwa kufanikisha mkutano huo wakiwa wanapitia vikwazo vingi, ikiwamo vya kiuchumi na kisiasa, hasa Mwenyekiti wao Freeman Mbowe na wanachama wengine kuwekwa rumande kwa takriban miezi minane na watu kuingia bungeni bila ridhaa ya chama.

Alisema suala la kina Mdee na wenzake 18 kuvuliwa uanachama siyo jambo geni kwa kuwa walishafukuzwa mwanzo, wakakata rufani lakini uamuzi wa rufani umechukua muda mrefu kutolewa.

Alisema uamuzi huo wa CHADEMA unapaswa kupongezwa kwa uamuzi huo kwa kuwa ulifanywa kwa kufuata demokrasia ikiwamo kufanyika vikao rasmi vya chama.

Alisema uamuzi huo ambao haukufanywa na kiongozi bali wanachama kwa vikao rasmi vya chama unapaswa uigwe na vyama vingine.

"Hao wapongezwe na ndivyo vyama vingine viige, hata CCM waige, wasimsikilize mkuu fulani hamtaki fulani ndiyo anaondoka, hapana! Wanachama wawe na uhuru wa kuamua kipi kifanyike, iwe ni kufukuza au kuingiza," alisema.

Mwandumi pia alisema suala la kudai Katiba Mpya ni muhimu kwa sababu limechelewa kushughulikiwa.

"Tukumbuke kwamba hata Rais wa awamu ya kwanza, Mwalimu Julius Nyerere, alisema katiba hii haifai, akipewa dikteta ni hatari, katiba hii ni ya mwaka 1977 ilitungwa ndani ya chama kimoja, watu wa chama kimoja. Pia ilipofika mwa 1992 hatukupata katiba mpya ila kiliingizwa kipengele cha mfumo wa vyama vingi," alisema.

**MDEE, MBOWE**

Aliyekuwa mwanachama wa Chadema, Halima Mdee, alidai hakukuwa na uhuru wakati wa mkutano wa juzi hasa katika upigaji wa kura, akisisitiza kuwa kilichofanyika ni uhuni.

"Huwa nakwepa kuzungumza maneno makali kwa sababu naheshimu viongozi wangu, lakini sikujua kama CHADEMA kunaweza kufanyika uhuni kwa kiwango hiko. Nitaendelea kuwa CHADEMA vizuri tu, lakini kichofanyika pale ni uhuni wa kiwango cha hatari, hata Mbowe mwenyewe anajua," alisema Mdee.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, alijibu kauli hiyo kuhusu uamuzi uliofanywa usiku wa kuamkia jana na Baraza Kuu la chama hicho, waliouita wa kihuni, akiwataka na wao kuacha uhuni.

"Wajumbe wamekuja leo na wamefanya uamuzi wakishuhudia na kura zimepigwa mbele yao, waache mambo ya 'kihuni'," Mbowe alijibu.

Mbali na Mdee, wengine waliovuliwa uanachama ni Grace Tendega, Ester Bulaya, Agnesta Lambert, Jesca Kishoa, Ester Matiko, Salome Makamba na Nusrat Hanje.

Pia wamo Tunza Malapo, Conchestar Rwamlaza, Naghenjwa Kaboyoka, Hawa Mwaifunga, Stella Fiao, Anatropia Theonest, Asia Mohammed, Sophia Mwakagenda, Cecilia Pareso, Kunti Majala na Felister Njau.

Katika upigaji wa kura, jumla ya wajumbe 423 walishiriki. Kati yao 413 (asilimia 97.6) walikubaliana na uamuzi wa kamati kuu kuwavua uanachama, watano (asilimia 1.2) hawakukubalina na uamuzi wa kuwafukuza huku wasiofungamana na upande wowote wakiwa watano (asilimia 1.2).

**VITI VYEUPE BUNGENI**

Kwa siku mbili juzi na jana, upande waliokuwa wanakaa wabunge wa viti maalum (CHADEMA) bungeni hawakuwapo, huku Mbunge wa Nkasi Kaskazini kupitia chama hicho, Aida Khenani, akionekana peke yake.

Hata hivyo, Nipashe lilimtafuta Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi ili kufahamu endapo Bunge limeshapokea barua kutoka CHADEMA inayoeleza kuwavua uanachama wabunge hao, lakini jitihada hizo ziligonga mwamba kutokana na kutompata kiongozi huyo kwa njia ya simu, pia kwenda ofisini kwake.

Kuvuliwa uanachama kwa wabunge hao kukiridhiwa na Bunge, kutakuwa na uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) pamoja na ile ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) ambazo kwa mujibu wa Kanuni za Bunge zinapaswa kuongozwa na wabunge wa upinzani.

PAC ilikuwa ikiongozwa na Naghenjwa Kaboyoka wakati LAAC ilikuwa ikiongozwa na Grace Tendega.

■ **Imeandikwa na Jenifer Gilla (DAR) na Augusta Njoji (DODOMA).**

# Watuhumiwa uhalifu wazidi kukamatwa

**Na Romana Mallya**

OPERESHI ya kuwasaka vijana wanaofanya uhalifu mitaani, maarufu 'panya road', mkoani Dar es Salaam imewakamata watuhumiwa wengine 23.

Wiki iliyopita Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam kupitia kamanda wake, Jumanne Muliro, lilitangaza kuwakamata watu 31 wanaodaiwa kujihusisha na matukio ya unyang'anyi, kujeruhi na kuiba.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Kamanda Muliro alisema kuwa hadi Jumanne ya wiki hii, walikuwa wamewakamata watuhumiwa 23 wenye umri kati ya miaka 13 hadi 24.

"Katika mahojiano, Jeshi la Polisi limebaini baadhi yao hawakumaliza shule ya msingi kwa utoro na sababu nyingine," alisema.

Alisema kuwa baadhi ya eneo hilo ilifanikiwa kuvipata vitu vilivyoibwa na wahalifu hao zikiwamo runinga tatu na simu moja.

Kamanda Muliro alikemea vitendo vya baadhi ya watu wanaoleta taharuki kwa wananchi wakisambaza taarifa za matukio ambayo hayapo.

"Kuna wakati vijana wanaotoka kucheza mpira jioni wanaporejea nyumbani wakiwa kwenye makundi baadhi ya watu wamekuwa wakitumiana ujumbe kuwa ni makundi ya kihalifu yamezagaa mtaani.

"Wapo wanaotumiana ujumbe kuwa wamekutana na makundi ya uhalifu, tunaomba wananchi wanaotaka ufafanuzi wapige simu **0787 668306 au 0755009983,"** alisema.

HABARI KITAIFA



Mwakilishi Mkuu wa JICA Tanzania, Hideki Watanabe (wa pili kushoto), akipata maelezo kuhusu masuala ya uchapishaji wa magazeti kutoka kwa Mkurugenzi wa Biashara wa Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Ajay Goyal (kulia), alipotembelea ofisi za TGL, Mikocheni, mkoani Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mshauri wa JICA Tanzania, Raymond Msoffe na Mhandisi wa TGL, Christian Ngwapaula. **PICHA: CARLOS BANDA**

# Aweso aanika mikakati kumaliza kero ya maji

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amelieleza Bunge mikakati iliyopangwa na wizara yake kuhakikisha kero ya maji nchini inamalizika, ikiwamo uvunaji wa maji ya mvua hususani kwenye maeneo kame.

Aweso alibainisha hayo jana Bungeni jijini hapa alipokuwa akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2022/23 huku akitaja mkakati mwingine kuwa ni ujenzi wa miradi mipya ya maji kwenye miji 28.

Ili kufanikisha azma hiyo, Waziri Aweso aliliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 709.36 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo.

Aliutaja mkakati mwingine kuwa ni kukamilisha miradi ya maji inayoendelea, kuboresha usimamizi na uendeshaji wa huduma ya maji vijijini, kuongeza uhakika wa uhifadhi wa maji kwa kuimarisha kitengo cha uchimbaji wa visima na ujenzi wa mabwawa.

Aweso alisema mikakati mingine iliyopangwa na wizara kwa mwaka 2022/23 ni kukamilisha ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miradi inayoendelea kwa kuhakikisha inatekelezwa pamoja na kuanza ujenzi wa mabwawa ya kimkakati ya Kidunda na Farkwa.

"Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India kupitia Benki ya Exim - India inategemea kuanza ujenzi wa mradi wa kuboresha huduma ya maji katika miji 28 ya Tanzania Bara na mji mmoja visiwani Zanzibar kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 500.

"Hadi Aprili 2022, taratibu za kuwapata makandarasi wa ujenzi katika miji 24 zimekamilika na kwamba ujenzi wa miradi katika miji hiyo itatumia fedha za mkopo wa India na miji minne ya Mafinga, Makonde, Songea na Tarime-Rorya utekelezaji wake utafanywa kwa kutumia fedha za ndani. Mikataba ya ujenzi itasainiwa kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2021/22, " alisema.

Waziri Aweso alitaja miji hiyo ni Muheza, Wanging'ombe, Kayanga, Makonde, Njombe, Makambako, Manyoni, Songea, Sikonge, Chunya, Kasulu, Kilwa Masoko, Rujewa, Mugumu, Geita, Chato, Zanzibar, Singida Mjini, Kiomboi, Mpanda, Chemba, Mafinga, UramboKaliua, Pangani, Ifakara, Rorya/Tarime na Chamwino.

Alisema wizara itaendelea na utunzaji wa vyanzo vya maji ikihusisha kutambua, kuweka mipaka na kutangaza kwenye Gazeti la Serikali ili vyanzo hivyo vilindwe kisheria kwa kuwekewa mipaka na kutangazwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Pia alisema wizara yake inatarajia kutekeleza miradi ya maji kwa kutumia vyanzo vya uhakika ikiwamo maziwa makuu na mito mikubwa na kwamba serikali imepanga kujenga mabwawa makubwa ya kimkakati yakiwamo mabwawa ya Kidunda, Farkwa, Lugoda na Songwe.

"Aidha, serikali itaanza ujenzi wa Bwawa la Kidunda lililochukua muda mrefu kutekelezwa baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kutoa kibali. Vilevile, Serikali itaanza ujenzi wa Bwawa la Farkwa na mtambo wa kutibu maji baada ya kupata fedha za mkopo Dola za Marekani milioni 125.3 (Sh. bilioni 280) kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika," alisema.

Sambamba na ujenzi wa mabwawa makubwa ya kimkakati, alisema serikali imepanga kujenga mabwawa ya ukubwa wa kati 23 hususani kwenye maeneo kame kwa ajili ya uvunaji wa maji ya mvua, ili kuongeza uwezo wa nchi kuhifadhi maji na kuyasambaza kwa wananchi wengi.

Waziri alisema katika mwaka 2022/23, Wizara ya Maji pia imepanga kutekeleza miradi 1,029 ya maji vijijini, kwamba kati ya miradi hiyo 648 ni ile inayoendelea kutekelezwa na miradi 381 ni mipya, pamoja na ujenzi wa mabwawa 15 katika maeneo mbalimbali ya vijijini.

Alisema serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Oman imepanga kuchimba visima virefu 20 kwenye maeneo ya vijijini katika mikoa ya Dodoma (5), Morogoro (5), Pwani (5), Singida (5).

Aidha, alisema katika kuhakikisha wananchi wanaoishi kwenye maeneo ya kandokando ya maziwa makuu wanapata huduma ya majisafi, salama na ya kutosheleza.

Sambamba na hilo, alisema serikali imepanga kuanza ujenzi wa miradi ya maji katika vijiji 48 vinavyozunguka Ziwa Victoria na vijiji 37 katika Ziwa Tanganyika, pamoja na kutekeleza miradi 175 ya maji mijini.

# Wanawake watano wauawa, wanyofolewa sehemu za siri

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WANAWAKE watano wilayani hapa wameuawa kikatili na watu wasiojulikana huku watatu kati yao wakikutwa sehemu zao za siri zimenyofolewa.

Mauaji hayo yamefanyika katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita, hatua ambayo imesababisha wananchi kuingiwa na hofu juu ya usalama wao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini hapa, Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Claudia Kitta, alisema amesikitishwa na mauaji hayo ambayo yameonyesha taswira mbaya hasa kutokana na wanawake kuuawa na kunyofolewa viungo vyao.

"Inasikitisha kuona kwamba ndani ya miezi mitatu, wanawake watano wamekutwa wameuawa katika maeneo tofauti. Hali hii inasikitisha na inatishia usalama wa wananchi," alisema Kitta ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya.

Alisema jambo ambalo linashangaza ni kwamba aina ya mauaji ni moja huku sababu zikiwa hazijafahamika na kuongeza kuwa Jeshi la Polisi bado linaendelea na uchunguzi

Kutokana na mauaji hayo, Kitta alisema Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya inaendelea kuimarisha ulinzi ikiwa ni pamoja na kulinda mali za wananchi na kuhakikisha matukio hayo yanakomeshwa.

Kitta aliwataka wananchi wilayani hapa kushirikiana na polisi kuhakikisha wahusika wa matukio hayo wanakamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Alisema njia ya peke ambayo pia inaweza kutumika katika kuimarisha ulinzi na usalama ni kuanzisha ulinzi shirikishi ngazi za kata, vijiji na mitaa hatua ambayo alisema itasaidia kupunguza matukio ya mauaji yanayoendelea wilayani hapa.

Pia aliwataka wananchi kutoa taarifa polisi pale wanapowaona watu ambao hawawafahamu kwenye maeneo yao ili wafuatiliwe na kujua uhalisia wake.

Baadhi ya wananchi waliozungumza na waandishi wa habari kwa nyakati tofauti walisema vitendo hivyo vimesababisha hofu miongoni mwa wananchi hasa kinamama ambao mara kwa mara wamekuwa wakijishughulisha na uzalishaji mali wanaotoka nyumbani na kwenda kwenye shughuli zao na kurudi.

Ismaily Kalindimba, Diwani wa Migongo, alisema wanawake wawili kati ya hao wameuawa katika kata yake. Kutokana na mauaji hayo alisema kila kijiji kimeanzisha ulinzi shirikishi, maarufu kama sungusungu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Kamishna Msaidizi (ACP) Nicodemus Katembo, alisema hadi sasa watu wawili wanashikiliwa na jeshi hilo kwa tuhuma za mauaji hayo.

ACP Katembo pia alisema polisi wanaendelea na uchunguzi wa matukio hayo huku akiwataka wananchi watoe ushirikiano ili kuwapata watu zaidi wanaotuhumiwa kujihusisha na mauaji hayo.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA U J E N Z I , UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA.

**TANGAZO**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe 15.05.2022 hadi 29.05.2022 kampuni ya Spedag Interfreight itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka Holili kuelekea Moshi, gari hilo lenye namba za usajili:

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - Mita 21, Upana - Mita 4.3, Kimo -Mita 5.3**

3. Njia itakayotumika: Holili hadi Moshi kupitia Soweto, gari litasafiri muda wa mchana tu

**( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

FCS FOUNDATION FOR CIVIL SOCIETY

**MWALIKO WA KUHUDHURIA MKUTANO WA WADAU WA SEKTA YA ASASI ZA KIRAIA TANZANIA NCHINI TAREHE 17/052022 MPAKA 18/05/2022.**

Foundation for Civil Society (FCS) ni taasisi isiyo ya kiserikali iliyosajiliwa mwaka 2002 na kuanza utekelezaji mwaka 2003, ikiwa ni taasisi yenye kutoa ruzuku na kuimarisha uwezo kwa Asasi za kiraia nchini Tanzania kutekeleza miradi yenye kuboresha hali za wananchi. Mnamo mwezi Septemba 2021, FCS ilizindua Mpango Mkakati wa mwaka 2022 – 2026. Utekelezaji wa mpango huu utaanza rasmi mwaka huu 2022. FCS ina penda kuwaalika Asasi za Kiraia ikiwemo Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs),Asasi za kijamii (CBO) ,Vyama vya kitaaluma,Vyama vya wafanyakazi,Taasisi za vyombo vya habari ,Vyama vya ushirika2, Asasi za kidini vikundi pamoja na watu binafsi wenye uwezo na nia ya kuleta chachu ya mabadiliko bara na visiwani, kuhudhuria mikutano utakao fanyika kwa njia ya mtandao wa zoom kati ya Tarehe13/05/2022 mpaka Tarehe 17/05/2022.

**Malengo ya mkutano ni**

1. Kuhabarisha wadua wa sekta ya Asasi za Kiraia nchini kuhusu Mpango Mkakati mpya na maeneo ya vipaumbele kwa mwaka 2022/2024
2. Kuwezesha Mashirika, vikundi na watu binafsi kupata ufafanuzi kwa kina kuhusu utaratibu mpya wa Upatikanaji wa ruzuku za FCS
3. Kuwezesha Asasi za Kiraia nchini kufahamu jinsi ya kujisajili kupitia mfumo mpya wa kidigitali

Mikutano hii itafanyika Kikanda kama ilivyoainishwa katika mikoa hapo chini. Tafadhali zingatia Tarehe na Kanda ambayo Mkoa wako unapatikana.

**Kanda ya Kaskazini**
Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Dodoma, Singida, Tabora
Geita, Kagera, Mara, Mwanza, Shinyanga and Simiyu

**Kiungo cha kujisajili:**
**https://thefoundation-or-tz.zoom.us/webinar/register/WN_GsUwXAeoS_OC3ewKUIYjNw**

Tarehe: Mei 17 2022. Muda: Saa 2:30 Asubuhi – 06:30 Mchana

**Kanda ya Pwani**
Dar es Salaam, Lindi, Morogoro, Mtwara, Pwani
Mjini Magharibi, Kaskazini Pemba, Kaskazini Unguja, Kusini Pemba na Kusini Unguja

**Kiungo cha kujisajili:**
**https://thefoundation-or-tz.zoom.us/webinar/register/WN_Ad14pAcUQx-qh2TnXPHpTw**

Tarehe: Mei 18 2022. Muda: Saa 2:30 Asubuhi – Saa 06:30 Mchana

**Kanda Kusini**
Iringa, Mbeya, Njombe, Rukwa, Ruvuma, Songwe, Katavi and Kigoma

**Kiungo cha kujisajili:**
**https://thefoundation-or-tz.zoom.us/webinar/register/WN_VWmXuNbvQM6-5CwOHyTMIw**
Tarehe: Mei 18 2022. Muda: Saa7::30 Mchana – Saa10:30 Jioni

**Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia:**
**Simu: +255 754 005 708; tovuti: www.thefoundation.or.tz na mitandao yetu ya kijamii; Twitter @fctz na Facebook: Foundation for Civil Society**

# Wakili maarufu atangaza mbinu kuiendeleza TLS

**Na Jenifer Gilla**

MGOMBEA urais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) 2022, Wakili Jeremia Mtobesya, ametaja mambo matatu ambayo atayafanya kama akipata nafasi ya kuwa rais wa chama hicho kulingana na mpango mkakati uliopitishwa na wanachama.

Amesema jambo la kwanza, atahakikisha kuwa anarudisha mifumo ya kibiashara ikiwamo kurudisha idara ya maendeleo ya biashara na nyinginezo ili chama hicho kiwe na uhimilivu wa kiuchumi kwa kutegemea vyanzo vya nje vya mapato na si ada za wanachama kama.

"Sasa nikifanikiwa kwenye 'financial sustainability' (uhimilivu wa kifedha) nitahakikisha ile 'business development department' (idara ya maendeleo ya biashara) inarudishwa kwa sababu nimeshuhudia ikifanya kazi," alisema hivi karibuni alipohojiwa na gazeti hili.

Kingine, alisema atahakikisha chama kitawasaidia vijana wapya wa fani ya sheria kuanzisha shughuli na miradi ya kujiingizia kipato ili kujipunguzia ukali wa maisha.

"Tutakubaliana ama wapewe vifaa au fedha kisha baadaye wazirudishe ili wengine waje kuzitumia. Nafikiria njia ambayo itakuwa endelevu isifanyike kwa wakati mmoja," alisema.

Alisema pia atawasaidia vijana hao kufanya shughuli zao katika hadhi kama ya mawakili wengine ili kukihudumia chama ikiwamo kulipa ada na kufanya michakato ya kupunguza mzigo wa ada ya uanachama ili hata vijana hao waimudu ikiwamo ya kutafuta vyanzo vya mapato ya nje kama biashara.

Wakili Mtobesya alisema pia atahakikisha chama kinawasaidia mawakala kupata msaada wa kisheria katika mfumo ambao ni wa kistaarabu.

"Mawakili wetu mara nyingi tumewaona wakiingiliwa katika kazi zao. Wakati mwingine ni kweli wakili anakuwa katika mgogoro wa kisheria. Iwapo nitapata wasaa nitahakikisha tunawasaidia mawakili wetu katika hali yoyote, wakiwa katika mgogoro tunawatetea haki zao," alisema.

Kuhusu katiba mpya alisema ataendeleza mijadala na midahalo kwa sababu tayari suala hilo liko katika mpango kazi wa chama hicho na wanachama walishakubaliana liendelee kuwapo.

Kuhusu muda wa kuongoza chama hicho, alisema waheshimu muda uliowekwa wa mwaka mmoja, kikubwa ni anayepata nafasi ahakikishe anafanya vizuri na kuacha njia nzuri kwa anayekuja.

# Serikali na wadau wa utalii kuteta tija filamu Royal Tour

**Na Romana Mallya**

SERIKALI inakutana na wadau wa utalii, zikiwamo hoteli zilizosimama kutoa huduma, ili kuimarisha sekta hiyo inayotarajiwa kupokea watalii wengi kutokana na hamasa inayochagizwa na filamu ya Tanzania The Royal Tour.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Prof. Godius Kahyarara, alibainisha hayo jana wakati wa mkutano na waandishi wa habari uliofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam.

Mkutano huo uliitishwa kueleza tathmini ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan Uganda na Marekani.

Akizungumzia kuhusu shughuli za kiuchumi ambazo zilifungwa na sasa baadhi zimefunguliwa, Prof. Kahyarara alisema zilizofungwa hazikufungwa kwa sababu ya kiserikali bali wengi walikuwa wanadaiwa na benki.

"Arusha unafahamu kuna hoteli kama ile Ngurdoto, Naura Springs, kesho (leo) tutapata sababu za msingi (za kufungwa), kamati iliyofanya kazi kesho watatupa taarifa, kesho tutakuwa na muda mzuri wa kujibu hilo swali," alisema.

Prof. Kahyarara alisema serikali imejiandaa kuwapokea watalii kwa kuhakikisha wanawekeza katika eneo la kukidhi haja ya muda mfupi na wa kati wa uwekezaji.

"Tumejiandaaje, kesho (leo) tuna kikao kikubwa na wadau, tumeshapita kwa wadau wote tumekubaliana kila mtu ameangalia eneo lake ni vitu gani vinaweza kufanyika ndani ya muda mfupi.

"Wadau ni watu gani? Kwanza ni hoteli, siyo kweli kwamba hoteli zetu ni asilimia 100 wana mahesabu watasema, wenzetu wa utalii bado hatujafika asilimia 100, hivyo wakiongezeka leo au kesho, keshokutwa bado tuna nafasi," alisema.

Pia alisema wapo wawekezaji na wengine wameshasaini mikataba ambao wana teknolojia mbalimbali wanaona kwao ni fursa.

Kadhalika alisema upo ujenzi unaofanyika ndani ya muda mfupi ambapo wapo walioanza kuulizia vibanda na tenti ambapo kesho (leo) wanatarajia kukutana nao ili kusikiliza mipango yao.

"Fabricated buildings (majengo ambayo hayatumii saruji) tayari wameshajitokeza na wenyewe tutawasikiliza, kwa hiyo tutajiandaa kupitia michoro yao, utayari wao na muda wao," alisema.

Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas, alisema ni mapema kupima matokeo chanya ya filamu ya The Royal Tour katika sekta ya utalii ingawa mapokeo yake duniani ni makubwa.

Alisema filamu hiyo inakaribia kuonyeshwa katika runinga 300 kati ya 350 zilizoko Marekani ambapo kila ilikoonyeshwa kiwango cha watazamaji ni kikubwa kulinganishwa na zilizowahi kufanyika huko nyuma na tayari usambazaji nchini umeshaanza.

Akizungumzia mafanikio ya ziara ya Marekani, Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Zuhura Yunus aliyataja maeneo mengi yakiangazia mwelekeo mpya katika sekta mbalimbali zikiwamo kilimo, afya, elimu, utalii, uwekezaji na biashara.

Pia alitoa mrejesho wa mkopo wenye masharti nafuu ambao serikali imeomba kupitia Shirika la Fedha Duniani (IMF) ambao ulitakiwa ushughulikiwe kwa haraka kuwa tayari timu ipo nchini na ifikapo Alhamisi watajua majibu yote na dalili inaonyesha ni nzuri.

Akizungumzia mradi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima mpaka Bandari ya Hindi mkoani Tanga, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, alisema serikali imekamilisha kulipa fidia na hivi karibuni watatangaza ajira.

HABARI KITAIFA

# Wanafunzi 153, 220 wachaguliwa kujiunga kidato cha tano, ufundi

**Na Mary Geofrey**

WANAFUNZI 153,219 wakiwamo wasichana 67,541 na wavulana 85,678 sawa na asilimia 91.8 ya wenye sifa, wamechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano, vyuo vya ualimu na elimu ya ufundi kwa mwaka wa masomo wa 2022/23.

Akitangaza matokeo ya uchaguzi huo jana, Dar es Salaam, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, alisema wanafunzi 90,825 wakiwamo wasichana 43,104 wamechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule za sekondari 499 zikiwamo mpya 22 za serikali zinazoanza mwaka huu.

Bashungwa alisema kati ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha tano, wako wanafunzi wenye uhitaji maalum 481 ambao kati yao wapo wasichana 204 na wavulana 277.

Alisema kati ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga kidato cha tano, wanafunzi 41,401 wakiwamo wasichana 17,390 watajiunga kusoma tahasusi za sayansi na hisabati na wanafunzi 49,133 wakiwamo wasichana 25,508 watajiunga kusoma tahasusi za masomo ya sanaa, lugha na biashara.

Kwa mujibu wa Bashungwa, wanafunzi 1,880 wakiwamo wasichana 757 wamechaguliwa kujiunga na fani mbalimbali katika vyuo vitatu vya elimu ya ufundi, ambavyo ni Chuo cha Ufundi cha Arusha (ATC), Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) na Chuo cha Usimamizi wa Maendeleo ya Maji (WDMI).

Pia alisema wanafunzi 2,294 wakiwamo wasichana 1,127 wamechaguliwa kujiunga na vyuo vya afya ngazi ya stahahada na 2,674 wakiwamo wasichana 1,366 wamechaguliwa kujiunga na vyuo vya ualimu ngazi ya stashahada ya sayansi, hesabu na teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

Bashungwa alisema wanafunzi 6,457 wakiwamo wasichana 3,168 wamechaguliwa kujiunga na astashahada ya elimu maalum, awali, michezo, msingi na ualimu wa shule zinazofundisha kwa kutumia lugha ya kiingereza (English Medium).

Alisema wanafunzi 49,089 wakiwamo wasichana 18,019 wamechaguliwa kujiunga na kozi mbalimbali za astashahada na stashahada katika vyuo vya elimu ya ufundi vinavyosimamiwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET).

**ONGEZEKO LA UFAULU**

Bashungwa alisema kumekuwa na ongezeko la wasichana 7,555 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha tano na vyuo vya ufundi, ukilinganisha na mwaka 2021.

"Hata hivyo idadi hii bado ni ndogo ukilinganisha na wavulana. Ili kukabiliana na changamoto hii, wizara inaendelea kuboresha miundombinu ya shule ili kuhakikisha wasichana wengi zaidi wanajiunga na kidato cha tano.

"Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuwezesha ujenzi wa shule za wasichana 10 za mikoa na kila shule itachukua wanafunzi 300 kuanzia mwaka 2023," alisema Bashungwa.Pamoja na ufinyu wa nafasi za kidato cha tano na vyuo vya elimu ya ufundi, alisema wanafunzi 14,254 wakiwamo wasichana 3,901 na wavulana 10,353 wamekosa nafasi.

Alisema kati ya wanafunzi waliokosa nafasi 12,876 wana sifa za kujiunga na kitado cha tano na kwamba hali hiyo imetokana na ongezeko la ufaulu wa wanafunzi wanaotakiwa kujiunga na kidato cha tano na vyuo mbalimbali.

"Hakuna mwanafunzi atakayekosa nafasi wote wataenda shule na vyuo baada ya wanafunzi wa awamu ya kwanza kuripoti na baada ya ukamilishaji wa baadhi ya miundombinu katika shule na vyuo," alisema Bashungwa.

**MWISHO KURIPOTI**

Bashungwa alisema wanafunzi wote waliopangiwa shule na vyuo wanatakiwa kuripoti kuanzia Juni 13 hadi 30 mwaka huu na endapo mwanafunzi atachelewa kuripoti nafasi yake itachukuliwa na mwanafunzi mwingine aliyekosa nafasi.

"Na kwa kuzingatia uchaguzi wa wanafunzi wa kujiunga na masomo umefanyika kwa kuzingatia ufaulu na nafasi zilizoko katika shule, hakutakuwa na fursa ya kufanya mabadiliko yoyote ya shule kutokana na ukosefu wa nafasi kwenye shule husika," alisisitiza Bashungwa.

Bashungwa pia aliwataka wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa, kuhakikisha kuwa azma ya serikali ya kuwa na sekondari za kidato cha tano katika kila halmashauri inatekelezwa ili kuwezesha wanafunzi wote waliofaulu mitihani ya kidato cha nne kupata nafasi ya kuendelea na masomo ya kidato cha tano na sita.

# Mawakili kizimbani tuhuma za kughushi

**Na Grace Gurisha**

MAWAKILI wawili wa kujitegemea na raia mmoja wa Ufaransa, wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa tuhuma za kughushi nyaraka za nguvu ya kisheria.

Washtakiwa hao ni Bernad Bougault ambaye ni raia wa Ufaransa, Respicious Mukandala na Simphorian Kitare ambao ni mawakili.

Akisoma hati ya mashtaka jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Francis Mhina, Wakili wa Serikali Kija Elias alidai kuwa washitakiwa hao walighushi nyaraka Februari 18, 2020 katika mtaa wa Samora, jijini Dar es Salaam.

Alidai kuwa nyaraka hizo zilionesha kuwa Kapteni Phillipe Gerniers amemchagua Boulgault kuwa mwakilishi wake kisheria na wakala wake huku wakijua si kweli.

Wakili Elias alidai hati hiyo, ilionesha Gerniers amempa Boulgault mamlaka ya kufungua mashtaka kwa ajili ya mali zake zilizoko katika Hoteli ya Bagamoyo Beach au alipwe Dola za Marekani 80,000 kwa niaba yake huku wakijua nyaraka hizo si za kweli.

Alidai upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika, hivyo akaiomba mahakama kutoa masharti ya dhamana kwa washitakiwa kwa kuwa kosa linalowakabili lina dhamana.

Hakimu aliahirisha hesi hiyo hadi Mei 23, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa na washitakiwa wote walipelekwa mahabusu kwa kushindwa kutimiza masharti ya dhamana.

Hakimu Mhina alisema ili washtakiwa wawe nje kwa dhamana, wanatakiwa kupeleka mdhamini mmoja mwenye barua ya utambulisho sambamba na kulipa Dola za Marekani 40,000 au kuepeleka hati ya mali yenye thamani hiyo.


NMB
Karibu yako

TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 22 WA WANAHISA WA BENKI YA NMB

**Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa 22 wa mwaka wa wanahisa wa NMB utafanyika katika ukumbi wa Julius Nyerere International Convention Centre, Dar es Salaam saa 4 asubuhi siku ya Ijumaa, Juni 3, 2022. Agenda itakuwa kama ifuatavyo:**

22.1 MATANGAZO NA AKIDI

22.2 KUPITISHA AJENDA ZA MKUTANO

22.3 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 21 ULIOFANYIKA TAREHE 4 JUNI 2021

22.4 YATOKANAYO NA MKUTANO WA 21 WA WANAHISA

22.5 KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA RIPOTI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA ZA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2022

22.6 KUIDHINISHA GAWIO KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2021

22.7 KUPOKEA NA KUIDHINISHA MALIPO YA WAKURUGENZI

22.8 KUJIUZULU NA UTEUZI WA WAKURUGENZI

22.9 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA UNAOMALIZIKA 31 DISEMBA 2022

22.10 MENGINEYO

**MAELEZO MUHIMU**

1. Mwanachama anayetarajia kuhudhuria Mkutano lazima aje na nakala yake ya risiti ya uwekezaji wa hisa (Depository receipt) au kitambulisho chake au kadi yake ya benki.
2. Mjumbe anayeruhusiwa kuhudhuria na kupiga kura kwenye Mkutano anaruhusiwa kuchagua mwakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata /kuzingatia taratibu na Sheria za Kampuni kama zilivyorekebishwa. Fomu ya uwakilishi lazima iwasilishwe kwenye ofisi iliyosajiliwa ya Kampuni kabla ya saa 4 asubuhi Alhamisi ya tarehe 2 Juni 2022.
3. Mwanachama anayetarajia kuhudhuria kikao atatakiwa kuhudhuria kwa gharama zake mwenyewe. Nakala za taarifa ya mwaka na fomu za mwakilishi zitapatikana matawini.
4. Wakurugenzi wamependekeza ulipwaji wa gawio la shilingi 193 kwa kila hisa, inayoleta jumla ya shilingi 96.7 bilioni kutokana na faida ya mwaka 2021.

**Tarehe za kuzingatia:**

| | |
|---|---|
| **Tarehe ya tangazo:** | - **13 Mei 2022** |
| **Hisa kuuzwa pamoja na gawio :** | - **13 Mei 2022** |
| **Mwisho wa hisa kuuzwa pamoja na gawio :** | - **1 Juni 2022** |
| **Hisa kuanza kuuzwa bila gawio:** | - **2 Juni 2022** |
| **Daftari la wanahisa kufungwa:** | - **6 Juni 2022** |
| **Malipo ya gawio kwa wanahisa: kuanzia tarehe** | - **15 Juni 2022** |

Lilian R. Komwihangiro
**Katibu wa Kampuni**

13 Mei 2022

www.nmbbank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua madhubuti zichukuliwe kudhibiti matukio ya uporaji

**MATUKIO** ya wizi, uporaji na ujambazi wa kutumia silaha yanazidi kuongezeka kwenye miji na majiji nchini, huku yakihusisha watoto na vijana wadogo wenye umri wa miaka minane hadi 17, maarufu kama 'Panya Road'.

Kutokana na matukio hayo, wako waliopata ulemavu wa kudumu, wengine wako hospitalini wanauguza majeraha na waliopoteza mali kwa kushambuliwa na vikundi hivyo. Vijana hao wameitwa jina hilo kutokana na umri wao kuwa mdogo na wanaweza kupenya kokote na kuchukua chochote kwa maelekezo ya wakubwa wao.

Wiki iliyopita, Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam lilitangaza kukamata vijana wa 'Panya Road' miongoni mwao wakiwa watoto wa umri wa miaka minane ambao hata wazazi au walezi wao hawakujua kama wanajihusisha na mambo hayo. Vijana hao walipobanwa na polisi, walikiri kuingia kwenye nyumba za watu kuiba na kupora mali zikiwamo fedha.

Kwa sasa matukio ya uporaji kwa kuvizia watu wakiwa nje ya malango ya kuingia nyumbani, barabarani na utapeli mwingine, yanaongezeka na karibu kila mtaa.

Mathalani, juzi ulisambaa ujumbe wa tahadhari kwa wakazi wa Tabara, Mabibo External na Kinyerezi kuwa kuna kikundi cha 'panya road' kinatembea mtaa hadi mtaa kupora watu. Ujumbe huo uliwataka wananchi kuchukua tahadhari kwa kujifungia ndani ya nyumba zao.

Kwa ujumla, uwapo wa watoto hao kama wahalifu, unaashiria kuna mahali walezi na wazazi wamepotoka. Hii inamaanisha kwamba wako watoto walioamua kujilea kwa miaka mingi kutokana na ombwe la malezi kutoka kwa wazazi wao. Hatua hiyo inasababisha hata familia kutokuuliza vijana hao wanatoa wapi fedha au mali walizo nazo, wanazozipata kutokana na uporaji.

Kutokana na tatizo hilo, ni vyema wazazi wajitathmini katika malezi ya watoto. Ni jambo la kushangaza kusikia mtoto wa miaka minane anajihusisha na vitendo vya uhalifu tena akiwa kwenye magenge ya kutisha kama 'panya road'.

Pamoja na kwamba tunaweza kuona mamlaka inayohusika na ulinzi wa raia na mali zao, yaani Jeshi la Polisi, halijatimiza wajibu wake vizuri kwa kuwa kwa intelijensia iliyopo wanapata taarifa nyingi ndiyo maana kunapotokea uhalifu wanajua kwa haraka na wanakamata na wanapofanya hivyo hali inatulia mitaani.

Tunaamini pamoja na jitihada za jamii, polisi wana nafasi kubwa ya kukabiliana na hali hii kwa kuwa wanafahamu mtandao wa matukio haya. Kwenye baadhi ya mitaa mtu akiibiwa anapokwenda polisi wakiamua kufuatilia, huwakamata na mali husika inarudi kirahisi. Hii inamaanisha kwamba polisi wanajua watu wanaofanya matukio hayo kirahisi.

Wakati tukiwataka polisi kutimiza wajibu wao, pia tuwatake warejeshe mkakati wa kuhamasisha wananchi kuunda polisi jamii ambao waliasisiwa na aliyekuwa Mkuu wa jeshi hilo, Said Mwema, ambaye alihakikisha kila mtaa una watu ambao walifanya vizuri sana, ingawa wako waliokengeuka na kuanza kufanya uhalifu kwa mwavuli wa polisi jamii.

Ni muhimu kwa serikali za mitaa kufanya vikao vya namna ya kuimarisha ulinzi wa maeneo yao. Yako maeneo yamefanya hivyo na kufanikiwa kudhibiti matukio ya uhalifu, hivyo tunaimani kwa kufanya hivyo kutakuwa na mafanikio makubwa kudhibiti matukio haya ya uporaji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kukimbia masoko machinga kutafutiwe ufumbuzi kamili

**KATIKA** biashara ya wamachinga, kuna mtindo ambao wamezoea kuufanya na unaendelea kuota mizizi kila kukicha, lakini ninadhani unaweza kuisababishia serikali hasara, iwapo hautadhibitiwa haraka.

Mtindo huo ni wa kususa masoko wanayojengewa na halmashauri ili kufanyia biashara katika mazingira mazuri, badala yake wao wanaamua kuyatelekeza na kwenda kandokando ya barabara.

Halmashauri zimekuwa zikijitahidi kuhakikisha zinajenga masoko mengi kwa ajili yao ambayo pia yatasaidia kuepusha na ajali za magari wanaweza kukumbana nazo wakiwa katika maeneo ambayo si rasmi kwa biashara.

Pamoja na juhudi hizo, vipo vikwazo hivyo vya kutohamia katika masoko hayo, ambavyo ninadhani kuna haja ya kuvitafutia ufumbufu wa kudumu, ili kinachofanywa na serikali kwa ajili ya kundi hilo kitimie.

Kwanza kabisa, ninaamini kuwa serikali inatumia gharama kubwa kujenga masoko hayo, lakini cha kushangaza ni huo mtindo waliojengewa wa kutotumia masoko hayo kana kwamba hayakutumia gharama yoyote.

Mkoani Dar es Salaam, yapo baadhi ya masoko ambayo wamachinga wameyakimbia, miongoni mwake likiwa ni soko la Mawasiliano ambalo uongozi unaomba wafanyabiashara wengine wajitokeze wepewe vizimba.

Hivi karibuni uongozi wa soko hilo ulieleza kuwa wamachinga wametelekeza vizimba vyao sokoni hapo na kurudi barabarani kufanya biashara kwa kupanga chini bidhaa zao, jambo ambalo linapingana na agizo la serikali.

Si hapo tu bali hata soko jipya la wamachinga lililojengwa pembeni mwa Stendi ya Magufuli, Mbezi Luis, nalo vizimba vyake viko wazi kufuatia wafanyabiashara hao kurudi barabarani.

Wengi wao wana vizimba katika soko hilo, lakini hawavitumii kutokana na kile wanachodai kuwa hakuna biashara, hivyo wanaona ni bora wawe kando ya barabara kupata wateja wakiwamo wapita njia.

Kwa mtindo huo, binafsi ninaona kama unachangia kuipa serikali, kwani ni wazi inatumia fedha nyingi ambazo ni fedha za walipa kodi kujenga masoko, lakini mwisho wa siku walengwa hawayatumii.

Ninadhani kwamba umefika wakati sasa wa kutafakari na kuchukua hatua ambazo zitasaidia masoko hayo kufanya kazi lakini bila kuumiza upande wowote, uwe wa wamachinga au serikali.

Ukiangalia juhudi zilizochukuliwa na serikali hasa mkoani Dar es Salaam za kuwaondoa wamachinga kwenye maeneo yasiyo rasmi, ni kama zimeanza kuvurugwa kufuatia wengi wao kurudi kule walikoondolewa.

Walianza kama mzaha vile kwa kurudi wachache katika maeneo walioondolewa, hasa wakati wa jioni, lakini sasa ninaweza kusema kuwa wamerudi rasmi badala ya kufanya biashara katika masoko waliojengewa.

Nadhani itakuwa vyema na busara sasa, kutafuta chanzo cha tatizo ili kukipatia ufumbuzi wa kudumu, hasa kwa kuzingatia asili ya biashara yao kuwa ya wanaotembea, huenda ikawa sababu ya kuwawia vigumu kukaa sokoni.

Lakini ingekuwa ni vyema wakatulia sehemu walizopangiwa, kwani wateja watawafuata huko badala ya kupanga bidhaa chini huku wakiacha mazingira mazuri ya kufanyia biashara ambayo wamejengewa.

Ikumbukwe ujenzi wa masoko hayo ni kuboresha na kutengeneza fursa zaidi shughuli za kundi hilo, kwani maeneo salama yanayotambulika na yanaweza kutumiwa na taasisi za kifedha kutoa mikopo na fursa nyingine za kiuchumi.

Ni wazi kwamba wamachinga ni wanufaika wakubwa wa masoko hayo, hivyo ingekuwa vyema iwapo wangeachana na mtindo wa kuyakwepa na kusababisha fedha za walipa kodi kupotea bure.

# Wanafunzi waliorejea toka nje kupangiwa vyuo kumalizia kozi

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameagiza wanafunzi waliokuwa wanasoma vyuo vya nje na kurejea nchini kutokana na mlipuko wa UVIKO-19 na vita vya Russia na Ukraine kwenda Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), wakafanyiwe tathmini na kupangiwa vyuo vya kusoma nchini.

Alitoa taarifa hiyo jana bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Hai (CCM), Saashisha Mafuwe, aliyetaka kufahamu hatima ya wanafunzi hao ambao walirudi nchi kutokana na majanga hayo.

"Wanafunzi wengi wapo hapa nchini wamekimbia vita vya Urusi na Ukraine, wengine walirudi kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona, wamesitisha masomo na wengine wanasoma kwa njia ya mtandao. Nini kauli ya serikali kwa waliokosa masomo?" Alihoji.

Akitoa ufafanuzi wa suala hilo, Waziri Mkuu Majaliwa alisema kwa wanafunzi ambao kozi walizokuwa wanasoma kwenye nchi husika haziendani na kozi zinazotolewa nchini wanapaswa kuwasiliana na TCU ili washauriwe kozi zipi za kuendelea kusomea nchini.

Hata hivyo, Waziri Mkuu Majaliwa alikiri kuwapo kwa vijana wa kitanzania waliokuwa wanasoma kwenye vyuo mbalimbali nje ya nchi na kutokana na UVIKO-19 na vita vya Ukraine walirejeshwa nchini.

Alieleza hatua ambazo serikali imeshazichukua katika kuokoa muda ambao wanafunzi hao wamepoteza kwenye masomo ni kutoa tangazo lililoratibiwa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Nchi na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia la kuwataka wanafunzi hao kuwasiliana na TCU.

Wanafunzi hao, alisema wakiwa TCU wanatakiwa kuelezea elimu yao na kipindi walichofikia katika masomo yao, ili taasisi hiyo ichukue alama zao na kuendelea na vyuo vya ndani.

Majaliwa alisema TCU itakachokifanya ni kufanyia tathmini viwango vya alama za kozi zao na ufaulu kuendana na alama za ndani, kisha kuwapangia vyuo vya kuendelea na masomo yao nchini.

"Sasa kama wako vijana ambao wamerudi na utaratibu huu hawakuupitia watakuwa hawajaripoti TCU au kozi anayoisoma haifanani na kozi zinazotolewaTanzania, kozi zetu zina vigezo na kiwango kinawezekana watakuwa na kozi hazifikii vigezo vyetu," alisema Majaliwa.

Alisema kwa wanafunzi wenye tatizo hilo la kozi zao kutoendana na kozi zinazotolewa nchini, wawasiliane na TCU ili washauriwe nini cha kufanya na kuendelea na masomo yao nchini.

# Aagiza elimu ya sensa itolewe kwa wananchi

**Na Munir Shemweta,** TANGA

KATIBU Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Allan Kijazi, amewataka maofisa Habari na Mawasiliano Serikalini kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa Sensa ya Watu na Makazi iliyopangwa kufanyika Agosti 23, 2022.

Dk. Kijazi alitoa agizo hilo jana mkoani Tanga alipowasilisha mada kuhusiana na Sensa ya Watu na Makazi kwenye kikao cha Maofisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano Serikalini kinachoendelea mkoani Tanga.

"Ninyi Maofisa Habari mnatakiwa kuelimisha wananchi umuhimu wa taarifa za majengo na ni kwanini ifanyike wakati huu," aliagiza Dk. Kijazi.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu huyo, ni vizuri maofisa habari wakashiriki vyema katika suala hilo kwa kutoa elimu sambamba na kubainisha kero na kutoa mrejesho hata kabla ya kuanza kwa sensa yenyewe.

Dk. Kijazi alisema takwimu zitakazopatikana wakati wa sensa zitaisadia serikali kupanga na kutekeleza mipango yake itakayoleta mabadiliko katika maendeleo ya kiuchumi.

"Ninaomba nitoe rai kwa wananchi, waiamini serikali yao kwa kuwa zoezi hili la sensa ya watu na makazi litaiwezesha serikali kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo itakayoleta mabadiliko katika uchumi, vinginevyo hatutapata takwimu sahihi," alisema Dk. Kijazi.

Aliongeza kuwa lengo la sensa ni kuiwezesha serikali kuwa na benki ya taarifa za makazi sambamba na kuhakikisha inakuwa na mikakati ya kujua makazi na kujua miji na vifaa vilivyotumika. "Kama nchi, lazima tuzingatie mikakati kulingana na takwimu zilizopo na hii ni sensa ya kwanza ya makazi," alisema Dk. Kijazi.

Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi 2022, Anna Makinda, alisema upo mkakati wa elimu na uhamasishaji kuhusiana na sensa na Maofisa Habari wa Serikali wanalo jukumu la kuhamasisha umuhimu wa sensa.

"Kila aliyekuwa serikalini lazima azungumzie sensa na maofisa habari ndiyo wenyewe na mkasaidie kuhamasisha hasa katika mitandao ya kijamii kwa kuwa wanaosoma zaidi mitandao ni vijana," alisema Spika mstaafu huyo.


## JOB VACANCIES ANNOUNCEMENT

### PHARMACEUTICALS AND MEDICAL DEVICES SALES REPRETATIVES

We are a Pharmaceutical, and Medical Devices Company. We import and distribute Pharmaceuticals and Medical Devices from Europe, Asia and other parts of the global.

We are looking for the qualified, motivated, people-oriented candidates to fill the job vacancies listed below in our company. The Pharmaceuticals and Medical Devices Sales Representative will be responsible for sales, promotion and marketing of our products. We also looking for a Biomedical Technician who will do the Repairs, services and installations of Medical Equipment.

**Job Title**

**1. Pharmaceutical Sales Representatives**

| Work Place | Number of Post |
|---|---|
| Arusha | 2 Posts |
| Dodoma | 2 Posts |
| Mwanza | 2Posts |
| Morogoro | 1post |
| Mbeya | 2 Posts |
| Zanzibar | 1 Post |
| Moshi | 1 Post |
| Dar es Salaam | 5 Post |

**2. Medical Devices Sales Representatives**

| Work Place | Number of Post |
|---|---|
| Dar es Salaam | 1 post |

**3. Biomedical Technician/Engineer**

| Work Place | Number of Post |
|---|---|
| Dar es Salaam | 1 Post |

**Key Requirement and Qualifications**

1. Diploma or Degree in the relevant field
2. Relevant Job Experience of more than two years.
3. The applicants must be willing to travel with little notice and havea good working knowledge of Tanzania regions.
4. Applicant should have good English and Kiswahili communication skills that will enable them to:

(i) Work on development and implementation of key marketing programs.
(ii) Provide Market updates, expense reporting and other required business reporting
(iii) Develop customer relationships and maintain a high level of customer satisfaction.
(iv) Proactively prospect for new customers and new opportunities.
(v) Solve a broad range of problems of varying scope and complexity.
(vi) Provide prompt response to all customer requests.
(vii) Applicant should have record of accomplishment of achieving sales targets around quota and sales forecastsand proactively drive the salescycle and forecastsales.
(viii) Applicant should have excellent computer skills to be able to make reports and presentations.
(ix) Applicant should be able to demonstrate

**Core Values of:** Innovation, Trust, Respect, Teamwork, Uncompromising Integrity, Speed, Focus and Accountability

**Mode of Application:**

**To apply, kindly submit your application with a detailed CV, photocopies of academic and other relevant certificates and names of three referees with their contacts to The Advertiser, P.O BOX 40385, DAR ES SALAAM, within two weeks form the date of this advertisement.**

**Please indicate your preferred work Station**

**Only short listed candidates with proven requirements and experience will be contacted.**

# Ofisi ya TPA Uganda kuanza kutoa huduma hivi karibuni

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Eric Hamissi amesema TPA inaitazama Uganda kama fursa muhimu ya kiuchumi kwa Tanzania kupitia huduma za kibandari.

Mkurugenzi mkuu Hamissi ametoa taarifa hiyo katika ofisi mpya ya TPA Nchini Uganda iliyopo Kampala iliyo katika hatua za mwisho kuanza kutoa Huduma
Kuanzishwa kwa ofisi hiyo kumelenga kuongeza ushawishi wa matumizi ya Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mwanza katika kuhudumia Shehena za Nchi ya Uganda kwa kupitisha malighafi za viwandani na kuwezesha bidhaa zinazozalishwa Uganda kufika katika Masoko sehemu mbalimbali duniani

Mkurugenzi mkuu wa TPA na Maafisi Waandamizi wa TPA wameshiriki katika ziara ya siku mbili ya Rais wa Tanzania Mhe Samia Suluhu Hassan Nchini Uganda.

Katika siku ya pili ya ziara yake Nchini Uganda, Mhe Rais Samia Suluhu Hassan ametembelea Makao Makuu ya Kampuni ya Roofing Group inayoongoza kwa kuzalisha vifaa vya ujenzi Nchini Uganda na kuwa na Masoko katika nchi mbalimbali barani Afrika.

Katika ziara hiyo, Rais Samia alielezea utayari wa Tanzania kushirikiana na taasisi za Uganda katika kukuza biashara baina ya nchi hizi mbili na kuikaribisha Kampuni ya Roofing Group kufanya uwekezaji Nchini Tanzania na kuahidi kuipa Kampuni hiyo ushirikiano wa hali na Mali ili Tanzania nayo inufaike na fursa zinazoambana na uwekezaji huo.

Mwenyekiti Mtendaji wa Roofing Group, Dkt Sikander Lalani aliishukuru Tanzania kwa kuwezesha biashara ya kampuni hiyo kufanyika kwa ufanisi kupitia hduma za bandari za Dar es Salaam na Mwanza; Shirika la Reli Tanzania , Kampuni ya huduma za Meli MSCL (TRC) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Roofing Group na Kampuni za Uchuzi za Tanzania zilisaini makubaliano ya kibiashara( SLA) Mwezi Februari 2022, makubaliano yanayotajwa kuongeza kiwango cha shehenza za Uganda zinazopita Nchi Tanzania kutoka 2% ya sasa hadi kufikia wastani wa 30%

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Masoko na Uhusiano TPA, Nicodemus Mushi alisema kuwapo kwa



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Mwenyekiti Mtendaji wa Kampuni ya Roofing Group ya Uganda Dkt Sikander Lalani mara baada ya ziara ya Mhe Rais katika Makao Makuu ya Kampuni hiyo Jijini Kampala.



Mkurugenzi kuu wa TPA Eric Hamissi

ofisi hiyo kutawezesha huduma za kibandari kupatikana kwa ukaribu zaidi nchini humo.

"Kuwapo kwa ofisi mpya mjini Kampala tunaongeza uwezo zaidi wa kuhudumia wateja wetu toka pale walipo nchini mwao na hivyo kurahisisha shughuli zote za kuhudumia shehena iwe inaingia au inatoka Uganda kupitia bandari zetu nchini Tanzania," alisema Mushi.

Ufunguzi wa ofisi hiyo ni mwendelezo wa juhudi kubwa zinazofanywa na TPA kuimarisha matumizi ya bandari za Tanzania kwa Nchi Jirani ambazo hazina bandari. Tayari TPA ina ofisi Kigali (Rwanda), Bujumbura (Burundi), Lubumbashi (DRC) na Lusaka (Zambia).

Mushi alisema katika kuhakikisha ofisi ya TPA nchini Uganda inafunguliwa, TPA inashirikiana kwa karibu na balozi za Tanzania Nchini Uganda ambaye ni mtekelezaji mkuu wa dhana ya Diplomasia ya kiuchumi ambayo jukumu lake kubwa ni kufanikisha biashara kati ya Tanzania na mataifa jirani.

"Mabalozi wetu katika nchi hizo shughuli zao nyingi zina uhusiano na shughuli za bandari na lojistiki. Wakati mabalozi wetu wanashughulika na diplomasia ya kiuchumi, sisi TPA tutakuwa tunajihusisha na usafirishaji, lojistiki na uwezeshaji biashara," alisema Mushi ..

Uamuzi wa kufungua ofisi mjini Kampala ni matokeo ya ziara ya siku tatu ya Rais Yoweri Museveni wa Uganda Nchini Tanzania mwaka jana. Katika ziara hiyo, Rais Museveni alipata nafasi ya kutembelea Bandari ya Dar es Salaam.

Rais Samia na Rais Museveni walikubaliana kuwapo kwa haja ya kufungua ofisi ya TPA Kampala ili kurahisisha usafirishaji wa mizigo kutoka Bandari za Dar es Salaam , Tanga na Mwanza hasa kipindi hiki cha ujenzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani, Tanga, Tanzania.

Mushi alisema uwapo TPA mjini Kampala pamoja na kunatarajiwa kuharakisha usafirishaji wa bidhaa na huduma zinazohitajika katika ujenzi wa bomba jipya la mafuta; pia kutarahisisha gharama ya kufanya biashara kati ya Tanzania na Uganda huku Bandari ya Mwanza ikitumika kupitisha Sukari ya Uganda kufikia Masoko ya Tanzania na Nchi nyingine Jirani.

TPA katika kuhakikisha bandari za Ziwa Victoria zinawezeshwa kushindana kibiashara, imefanya ukarabati wa bandari ya Mwanza Kusini maalumu kuhudumia meli za mizigo na bandari ya Mwanza Kaskazini inayojihusisha na shughuli za abiria.

Maboresho hayo yamesababisha usafirishaji wa mizigo kutoka Dar es Salaam kwenda Uganda kupitia ukanda wa Kati wa Tanzania kuwa bora zaidi na kuwezesha kukua kwa biashara kati ya Tanzania, Uganda na Sudan Kusini.
Maboresho ya Bandari ya Mwanza Kusini ilihusisha pia kufufua mfumo wa usafirishaji makasha hadi Port Bell nchini Uganda na maeneo mengine kwa kutumia vivuko vya mabehewa.

Njia ya kati ya reli kuanzia Bandari ya Dar es Salaam -Mwanza - Port Bell ni moja ya njia za kuaminika za kusafirishia shehena na ina gharama nafuu zaidi kuliko njia zote.

Mushi alisema TPA inafanya kazi kwa karibu na TRC na MSCL ili kwa Pamoja kuweka mifumo bora ya usafirishaji wa mizigo kutoka na kuingia Uganda kupitia Bandari za Tanzania.

"Msisitizo wa Serikali ya Awamu ya Sita ni kuongezeka kwa shehena ya mizigo ya Uganda inayopitia bandari zetu za Dar es Salaam, Tanga na Mwanza na tunatekeleza maagizo ya serikali na kuhakikisha tunaingia kwenye soko la Uganda na hivyo na kukuza uchumi," aliongeza Mushi.

Shehena ya Uganda kupitia bandari ya Dar es Salaam iliongezeka hadi tani za metriki 191,282 mwaka 2020/2021, kutoka tani metriki 140,269 zilizorekodiwa mwaka uliopita.



Bandari ya Dar es Salaam eneo la kuhudumia Makasha



Bandari ya Tanga



Bandari ya Mwanza

# Watanzania kunufaika mafunzo gesi, mafuta

**Na Getrude Mbago**

WATANZANIA wanatarajiwa kunufaika na elimu kuhusu sekta ndogo ya mafuta na gesi asilia itakayotolewa na wataalamu wa Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) kwenye maonyesho ya Nne ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi mkoani Morogoro.

Wataalamu hao wamejipanga kukuza uelewa wa sekta hiyo ili kuongeza ushiriki wa Watanzania kwenye miradi mbalimbali inayotekelezwa kwenye sekta husika.

Maonyesho hayo yalifunguliwa Mei 9 mwaka huu na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martin Shigella katika viwanja vya Jamhuri mkoani humo na yataendelea hadi Mei 14, mwaka huu, yakitarajiwa kuhitimishwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Baadhi ya masuala yatakayozungumziwa kwenye banda la PURA ni pamoja na mnyororo wa thamani wa mafuta na gesi asilia, mnyororo wa thamani wa mradi wa kubadili gesi asilia kuwa kimiminika (LNG) na shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia zinazoendelea nchini.

Maeneo mengine ni ushiriki wa wazawa kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ya mkondo wa juu wa petroli na fursa zinazopatikana kwenye utekelezaji wa miradi hiyo.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa maonesho hayo, Shigella alisema maonyesho hayo ni fursa kwa wafanyabiashara na wajasiriamali kujifunza na kubadilishana uzoefu wa kazi na washiriki wengine kuhusu fursa mbalimbali na kero zinazowakabili na jinsi ya kukabiliana nazo.

"Maonyesho haya ni ya muhimu kwani yanatoa elimu kwa wananchi ambayo inawawezesha kushiriki kwa wingi na kwa ubora kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo," alisema.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Beng'i Issa, alisema maonyesho hayo kwa mwaka huu yanaongozwa na kaulimbiu 'uchumi imara kwa maendeleo endelevu'.

Alisema lengo la maonyesho hayo ni kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu uwapo wa mifuko na programu za uwezeshaji, jinsi ya kujiwekea akiba na jinsi ya kuwekeza kwenye miradi ya maendeleo.

"Maonyesho haya pia yanalenga kutengeneza mtandao wa wafanyabiashara watakaoshiriki na kukuza masoko ya wajasiriamali ili kujiletea maendeleo," alibainisha.

# Tahadhari yatolewa ulaji nyama mbichi, maziwa yasiyochemshwa

**Na Stevie Chindiye,**
TUNDURU

UNYWAJI maziwa yasiyochemshwa na ulaji wa nyama zinazotokana na ndege ambazo havijaiva vizuri ni hatari kwa afya ya binadamu ikiwamo kuambukizwa magonjwa kikiwamo kifua kikuu (TB)

Mtratibu wa TB na Ukoma Wilaya ya Tunduru, Dk. Mkasange Kihongole, alisema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi waliojitokeza kupima afya ili kubaini kama wana maambukizi ya kifua kikuu, katika kijiji cha Muhuweni.

Dk. Kihongole alisema hali hiyo imetokana na kuwapo kwa taarifa za kitaalamu zilizothibitisha kuwa kuna aina ya ndege ambao huliwa na ng'ombe ambao hutoa maziwa na kutumiwa na binadamu, hivyo kuwapo uwezekano wa kupata TB kirahisi.

Kwa mujibu wa Dk. Kihongole, uchunguzi wa kitabibu unaonyesha kuwa asilimia 20 ya wagonjwa wa kifua kikuu huambukizwa kwa kutumia njia hizo huku asilimia 80 wakiambukizwa kwa njia ya hewa.

Kihongole alisema wazee, watoto, wanaotumia pombe kupita kiasi, wavutaji wa sigara na bangi, wako kwenye hatari kubwa kuambukizwa kifua kikuu sambamba na watu wanaoishi katika makazi duni na abiria wanaosafiri kwenye vyombo vya moto.

Alisema kutokana na uwapo wa viashiria hivyo miongoni mwa jamii inayoishi wilayani Tunduru, takwimu zinaonyesha kuwapo kwa idadi kubwa ya wagonjwa wa TB kwa kuwa katika kipindi cha mwaka 2021 pekee, ofisi yake ilibaini wagonjwa 765 katika vijiji vitano vilivyofanyiwa utambuzi.

Dk. Kihongole pia alisema kutokana hali hiyo, Wizara ya Afya ilianzisha Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma kwa kuanza kutumia kliniki inayotembea ikiwa ni jitihada za serikali kuwajali wananchi wake na kutokomeza.

Mpango huo, alisema unakwenda sambamba na malengo ya Shirika la Afya Duniani (WHO) yanayoelekeza kuwa ifikapo mwaka 2030 -2035 pasiwapo na TB na ugonjwa huo kubaki historia kama ilivyo kwa ugonjwa wa ndui ambao ulisumbua sana wakati wake.




Ofisa Mkuu wa Tigo Pesa, Angelica Pesha (kulia), akiwa ameshikana mkono na Meneja Mwandamizi Hazina, Masoko ya Hisa na Mitaji wa Benki ya Azania, Rukwaro Senkoro, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa bidhaa mpya inayoitwa "Bustisha", kwa ushirikiano na benki hiyo, itakayowawezesha wateja wa Tigo Pesa kukamilisha miamala yao hata kama hawana fedha za kutosha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# BMIA yazindua awamu II mafunzo habari za fedha

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Bloomberg Media Initiative Africa (BMIA) imetangaza kuanza kwa awamu ya pili ya programu ya mafunzo ya uandishi wa habari za masuala ya fedha (FJT) kwa waandishi nchini.

Mafunzo hayo yamelenga kuwawezesha jumla ya waandishi wa habari 50 wa masuala ya fedha na biashara kuandika habari za kina zinazohusu sekta hizo.

Awamu hiyo ya pili inafanyika baada ya mafunzo hayo kusimama kwa miaka miwili kutokana na shida ya changamoto za ugonjwa wa UVIKO-19.

Mafunzo hayo yanaendeshwa kwa ushirikiano kati ya Shule Kuu ya Biashara ya Strathmore ya Kenya, Shule Kuu ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDBS) na Shule Kuu ya Habari na Mawasiliano kwa Umma ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (SJMC).

Kurejewa kwa mafunzo hayo kunatokana na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika awamu ya kwanza iliyofanyika 2019 ambapo waandishi wa habari 40 walipata taaluma mbalimbali kuhusiana na uandishi wa habari za masuala ya fedha na biashara.

Katika awamu ya pili kutakuwa na waandishi wa habari 50 kutoka vyombo vya serikali, sekta binafsi, taasisi zisizokuwa za kiserikali na vyombo vikubwa vya habari.

Pia imeelezwa kuwa mafunzo hayo ya miezi sita yatahusisha mada mbalimbali zikiwamo uchambuzi wa data, masoko ya hisa, uhasibu, sera, uchumi na hivyo kuwezesha mabadiliko ndani ya vyombo vya habari ya namna ya kuandika habari za masuala ya fedha na biashara.

Mafunzo hayo yatatolewa na waandishi wa habari wa Bloomberg News na shule zilizotajwa. Mafunzo hayo yamelenga kuhakikisha kunakuwa na uwajibikaji, uwazi na utawala bora.

Mafunzo hayo ni sehemu muhimu ya BMIA kuchangia maendeleo katika uandishi wa habari za fedha na biashara barani Afrika, kwa kutambua umuhimu wa vyombo vya habari katika kuleta uwazi, uwajibikaji na utawala bora.

Akizungumzia mafunzo hayo, Mkurugenzi BMIA, Erana Stennett, alisema: "Tumefurahishwa na kurejea tena katika kutoa mafunzo ya programu baada ya miaka miwili. Tunaamini kwa kuwapa waandishi wa habari ujuzi na maarifa ili kuripoti vyema masuala ya biashara na fedha tunachangia ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Tanzania."

Akizungumza katika uzinduzi huo, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Profesa Florens Luoga, alisema: "Katika kipindi hiki kigumu baada ya janga la corona, uandishi thabiti wa habari za kibiashara na kiuchumi ni msingi mkubwa wa kuwafahamisha wadau ili kuwa na msukumo mkubwa wa ukuaji wa uchumi.

"Kwa kutoa mafunzo kwa wanahabari zaidi, BMIA inachangia maendeleo ya kiuchumi ya Tanzania."

Kuzinduliwa kwa awamu ya pili nchini kunafuatia kuwapo kwa mafanikio makubwa ya programu hiyo kwa nchi za Kenya, Nigeria, Afrika Kusini, Ghana, Zambia, Ivory Coast na Senegal, ambako zaidi ya waandishi 600 wamepatiwa mafunzo hayo.

# Serikali yatoa kibali ajira zingine maelfu

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, amesema Rais Samia Suluhu Hassan ameridhia kibali cha ajira kwa kada nyingine ikiwamo watendaji wa vijiji na kata.

Mhagama aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akiongezea majibu katika swali la nyongeza la Mbunge wa Mbulu Mjini (CCM), Zacharia Issaay.

Mbunge huyo alisema kada ya watendaji wa kijiji na mitaa hazijapata kibali ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ina upungufu wa watumishi hao kwa kipindi cha miaka mitatu sasa kwa zaidi ya asilimia 70.

"Serikali ina mkakati gani wa kuajiri watumishi hawa kwa Halmashuari ya Mbulu?" Alihoji.

Waziri Mhagama alisema Rais alitoa kibali cha ajira 32,604 za mwaka wa fedha 2021/22 na tayari ajira za kipaumbele kwa kada ya afya na elimu na nyingine ambatanishi zimetolewa.

Hata hivyo, alisema kada nyingine za ajira ikiwamo watendaji wa vijiji na kata zitafanyiwa mgawo kwenye ajira 7,792 ambazo zinasimamiwa na ofisi hiyo.

"Mheshimiwa Rais kupitia ofisi yetu ameridhia kada nyingine zilizobakia za watumishi ikiwamo watendaji wa vijiji na kata zifanyiwe mgawo kwenye ajira 7,792 ambazo bado zinasimamiwa na Ofisi ya Rais Utumishi," alisema.

Awali, akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alisema kwa sasa serikali imeshatangaza ajira kwenye kada ya elimu na afya za kipaumbele.

Hata hivyo, alisema ajira zingine zitaendelea kutangazwa kwa awamu ili kuhakikisha watumishi wa kada hizo wanaajiriwa na halmashauri zimeendelea kuajiri watendaji hao kwa kutumia mapato ya ndani.

Katika swali lake la msingi, mbunge huyo alihoji lini serikali itaajiri watumishi 40,000 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ilivyopitishwa kwenye Mpango na Bajeti wa mwaka 2021/22.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Dugange alisema katika mwaka wa fedha 2021/22 tayari serikali imekwishatoa Ikama na kibali cha ajira kwa halmashauri zote nchini.

Alisema nafasi za ajira za watumishi 17,412 wa kada ya afya na elimu zimetangazwa na taratibu za kuajiri watumishi hao zinaendelea kukamilishwa.

Alisema ajira za kada zingine zinaendelea kutolewa kupitia Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma na halmashauri husika.




Habari zote na Augusta Njoji



Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa, akijadiliana jambo na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Eliezer Feleshi, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Mbunge ataka mikakati kuvutia uwekezaji nchini

MBUNGE wa Kinondoni, Tarimba Abbas, ameitaka serikali kuweka mifumo rafiki ya kurahisisha ufanyaji wa biashara ili kuvutia zaidi uwekezaji nchini.

Akiuliza maswali bungeni jana, mbunge huyo alisema utekelezaji wa mifumo rafiki unasuasua huku akisema andiko la blue print (uchumi wa bluu) linaelekeza kutakuwa na mchanganuo wa jinsi ya kutekeleza na muda maalum.

"Je, serikali ipo tayari kuleta bungeni mchanganuo wa jinsi gani changamoto zake zinakwenda kutekelezwa na muda uliopangwa?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema utekelezaji wa blue print ulianza mwaka 2018 na bado kuna vikwazo vichache na kwamba kuna umuhimu wa kuhuisha.

"Na wabunge watapata kujua utekelezaji wake na muda uliopangwa," alisema na kubainisha kuwa hivi karibuni wizara itakuwa na vitengo kwenye halmashauri na kutakuwa na maofisa uwekezaji na biashara watakaoshirikiana na mamlaka ili kuendelea kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini.

Alisema serikali imeendelea kufanya maboresho ikiwa ni pamoja na kurekebisha sheria, kuweka mifumo ya kielektroniki, kufuta au kupunguza tozo na ada kero.

"Nyingine ni kuanzisha vituo vya pamoja vya kutoa huduma, kusogeza huduma karibu na watumiaji, kuboresha mifumo ya ukaguzi wa pamoja, kuweka utaratibu wa ukaguzi unaozingatia vihatarishi, kujenga uwezo katika mamlaka za uthibiti na kuweka taratibu na kanuni za kujidhibiti," alisema.

# Hospitali huduma za uzazi kujengwa

KUANZIA Julai mwaka huu, serikali itatekeleza mradi mkubwa chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia (WB) utakaogharimu Sh. bilioni 460 ambao unalenga kuboresha huduma za kinamama na watoto wachanga nchini.

Vilevile, serikali inatarajia kupitia fedha hizo kujenga hospitali ya kwanza ya kitaifa huduma ya mama na mtoto mkoani Dodoma.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alibainisha hayo jana bungeni alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Lucy Sabu.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema pamoja na jitihada zinazochukuliwa na serikali za kupunguza vifo vya wajawazito, bado kasi ya upunguzaji hairidhishi.

"Je, serikali imefanya tathmini ya sababu zake? Kwa kuwa vifo vya wajawazito vinatokana na uzazi pingamizi na majengo mengi yaliyojengwa ya upasuaji hayana wataalamu, serikali inatoa tamko gani juu ya jambo hilo?," alihoji.

Akijibu swali hilo, Waziri Ummy alisema kipaumbele cha serikali ni kuhakikisha inapunguza vifo hivyo.

"Niwahakikishie wabunge kwamba serikali ya awamu ya sita inayo mikakati mingine ya ziada ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi. Mwezi Julai inakwenda kutekeleza mradi mkubwa wa Sh. bilioni 460 chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia ambao unalenga huduma za kinamama na watoto wachanga," alisema.

Alisema katika mradi huo vitajengwa vyumba vya wajawazito na mahututi kwa hospitali za wilaya, kuwajengea uwezo watumishi wa afya ili kutoa huduma bora za uzazi wakati wa kujifungua.

"Tutaweka vifaa tiba pamoja na dawa za kuzuia vifo vya wajawazito, nimhakikishie mheshimiwa mbunge taarifa rasmi za vifo vitokanavyo na uzazi tutazipata Oktoba 2022 baada ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu kukamilisha utafiti kuhusu hali ya afya na demografia nchini, tutajua vinapungua kwa kiasi gani," alisema.

Awali, katika swali lake la msingi, mbunge huyo alihoji mpango wa serikali kupunguza vifo vya wajawazito.

Akijibu swali hilo, Waziri Ummy alisema serikali inatoa elimu kwa umma hususani kwa wajawazito kuhusu viashiria vya hatari kupitia njia mbalimbali ikiwamo vyombo vya habari na wakati wa mahudhurio ya kliniki.


Alisema serikali imesomesha wataalamu mbalimbali wa afya ya uzazi katika ngazi ya ubingwa na inaendelea kuimarisha miundombinu katika vituo na kuhakikisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba pamoja na kuhakikisha huduma za wajawazito zinatolewa bure.

Katika swali jingine la nyongeza, Mbunge wa Viti maalum (CCM), Lucy Mayenga, alihoji kwa nini serikali isifanye utafiti kujua sababu zinazosababisha kinamama wanaojifungua kwa oparesheni kupata maumivu ambayo yanawasababishia ulemavu mara baada ya kujifungua nchini.

"Kinamama wengi wanaojifungulia Tanzania wamekuwa wakilalamika maumivu makubwa sana wanayoyapata mgongoni kutokana na oparesheni walizofanyiwa, sasa kutokana na fedha hizo Sh. bilioni 460 za Benki ya Dunia, kwanini serikali isifanye utafiti kujua sababu zinazosababisha maumivu hayo nchini?" alihoji.

Waziri Ummy akijibu swali hilo, alisema fedha hizo zinajikita kuboresha huduma za uzazi, hivyo sindano hiyo ya usingizi watafanya utafiti na kusisitiza serikali inakwenda kuhakikisha inatumia huduma za ubingwa za uzazi kwenye mradi huo.

Ukurasa 13




Hivi kweli Uviko-19 unaishi kwa adabu?

BUFE
IJUMAA MEI 13, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



**TARI RASMI YAGONGA HODI... Kung'ara kwa walima tangawizi kitaifa Same na magonjwa 'kuwavuta shati'**

Ukurasa 14

# Waliokabiliwa na adha zote za umasikini na makazi, wazawadiwa nyumba mpya

## • Makazi yao na walivyoishi...Mungu anajua!
## • Mjane alipoonyeshwa jengo lake, alianguka

**Na Mary Mosha, MOSHI**

"UPEPO, baridi, jua, kurushiwa vitu vyangu nje, watoto wangu kurudishwa shule kwa pesa ya chakula na kuvaa nguo zenye viraka, haya yamekuwa ni maisha yangu mimi na wanangu, tangu mume wangu alipofariki mwaka 2017," anatamka Mwajuma Mbigiri.

Mjane mwenye watoto watatu mkazi wa kitongoji cha Mgohoroni, kijiji cha Mpirani, kata ya Mabogini Wilaya ya Moshi, mkoa wa Kilimanjaro anaendelea:

"Siku ya pili baada ya mume wangu kufariki na kuzikwa familia(wakwe) walitufukuza na kuchukua mali za mume wangu, ingawa zilikuwa ni kidogo, huku wakidai ndani ya ukoo wao hawawezi kupata mtoto mlemavu."

Mama huyo anafafanua mtoto wa kwanza ana umri wa miaka 17 anayesoma kidato cha nne, wa pili ana miaka 11, darasa la nne na wa mwisho miaka saba, ambaye ni mlemavu wa viungo, ndiye sababu kubwa yeye kufukuzwa na wakwe zake.

"Nimeishi maisha ya kuomba omba kulala barazani, mvua jua, upepo vyote vyangu na wanangu. Nilipojaribu kurudi nyumbani kwa wazazi wangu, pia walinikataa wakinitaka kuwarudisha watoto kwao, ili waweze kuniozesha kwa mwanaume mwingine," anafafanua Mwajuma, anayeunganisha sentensi zake na machozi.



Mwajuma Mbigiri, akifungua mlango wa nyumba mpya aliyokabidhiwa na Shirika la Tanzania Women Reseach Foundation (TAWREF) **PICHA: MARY MOSHA.**

Anasema wameishi maisha ya mateso, huku wakiomba nyumba za watu kulala, baadhi wanawapa ushirikiano, wengine wanawafukuza kwa madai ya kumkaribisha mlemavu nyumbani ni ishara ya mkosi.

Mwajuma anaeleza kwamba, baada ya kuteseka kwa muda mrefu, alibahatika kupata nyumba kutoka kwa msamaria mwema. Anafafanua: "Mabati yametoboka, kuta zote zina nyufa, mvua inaponyesha maji yanaingia ndani, ila kutokana na mateso ya muda mrefu niliifananisha nyumba ile na Ikulu.

"Tuliishi na wanangu kwa shida, huku tukibangaiza huku na kule kuona namna ambavyo tutapata chakula. Hakuna ofisi ya serikali sikuingia na kuomba msaada wa kisheria, kupata chakula na hata chakula kwa watoto wangu shule."

"Siku zote mvua zinaponyesha hasa nyakati za usiku, ilitulazimu kuamka kuchukua mwavuli na kumfunika mwanangu mdogo, huku tukiangalia mwelekeo wa maji na baada ya hapo tukisubiri mvua ikate na kuendelea na maisha," anasema

Anafafanua, mchana vumbi liliingia ndani kwa kukosekana madirisha, hivyo maradhi kama kikohozi na mafua hayakuisha, jambo ambalo kwake hakuliona tatizo kwani alizoea shida.

"Pamoja na hali hiyo ya nyumba, bado hatukuwa na choo. Hivyo tulilazimika kujisaidia kwenye ndoo na kutegea nyakati za mchana watu wakishaenda makazini na kumwaga kwenye vyoo vya watu, haikuwa rahisi!.

"Hadi hapo tulipopata msamaria mwingine ambaye alitusaidia choo kilichojaa tuendelee kukitumia kwa muda, ambako tulilazimika mtu kusukuma kinyesi kabla ya kujisaidia.

"Nilikwenda mashirika ya kutetea haki za watoto na wajane angalau nipate rasilimali za mume wangu na kupata pa kuanzia ilikuwa ni ngumu na mwisho nilikata tamaa na kumuachia Mungu.

"Kila mara nilikumbuka maneno ya marehemu mume wangu ya kunitaka kutowaacha watoto, hata kama nitapitia magumu kiasi gani," anasimulia Mwajuma, anayetaja magumu aliyopitia, zinajumuisha ushawishi aina nyingi kumtendea mabaya mwanawe mwenye ulemavu, kama namna ya kuondokana naye.

"Haya maisha nilikuwa nikiyasikia kama hadithi, lakini nimeyaishi kwa muda huu. Mungu mkubwa wakati mwingine nilipata wafadhili walilipa pesa kidogo," anaeleza.

### KILICHOFATA MAISHANI

Mwajuma, anaelezea kuna siku katika harakati za kuomba riziki kwa ajili ya wanawe, alisikia ipo taasisi inayoweza kuwasaidia watu ujenzi wa nyumba.

"Nilianza safari ya kwenda huko na kuomba msaada , ambako siku moja nikiwa nyumbani kwangu, walikuja wataalamu wa afya wanaotaka kupima afya zetu," anafafanua.

Mwajuma anaeleza mtaalamu aliumizwa sana na alichokishuhudia kwenye maisha yao na akataka kufahamu historia yao, hata akajuzwa na baada ya muda alirejea na wenzake waliotaka kupata eneo lao, wao wakikosa la kusema.

Mama huyo anasema, alianza kuwaomba watu wenye maeneo kumsaidia na akakutana na anayemtaja kwa jina Mzee Malisa, akawapatia eneo lake hatua za mita 20 kwa 14, hata akaweza kujengewa na kuishi na watoto wake.

### DAKTARI TAWREF

Azizi Mtawa, ni daktari wa shirika la TAWREF anasema, wakati anawajibikia majukumu yake, akapata taarifa za kuwepo mwenye shida eneo la Mabogini, wilaya ya Moshi na akafika aliko kupata hali halisi.

"Tulimkuta ana uhitaji zaidi wa chakula na dawa, niliangalia nyumba wanayoishi na kilikuwa ni kipindi cha mvua, maji yalikuwa mpaka ndani. Nyumba aliyokaa haikuwa na hadhi ya kuishi hata mnyama.

"Hakuna vitanda wala magodoro, hakuna choo nilipoondoka nikaondoka na mzigo mkubwa kama binadamu. Niliwakusanya marafiki zangu, tukaanza na

INAENDELEA UK.14

BIASHARA

### IJUE KAZI YA UTT AMIS

# Mkono wa Wizara ya Fedha unaofungua milango, dawa inayotibu magumu ya uwekezaji kwa wote

- Darasa kamili; fursa umri wowote; 'wadundulizaji' wamo

**Na Frank Monyo**

KUTOKANA na hali ya uchumi wa Dunia, kuna kundi kubwa la watu wanaojihusisha na biashara au ujasiriamali, wakilenga kujikimu na kuongeza kipato, lakini wako njia panda wafanye nini.

Wapo wengi wamejiunga na biashara ilhali hawana elimu sahihi ya fedha au namna ya kukabili changamoto katika uwekezaji.

Ofisa Mwandamizi wa Masoko na Uhusiano wa asasi ya UTT AMIS, Rahim Mwanga, anasema mifuko ya uwekezaji ni njia mojawapo sahihi ya kupunguza hatari au changamoto za uwekezaji.

Mwanga anaeleza: "Mwekezaji yeyote anahitaji njia sahihi za kupunguza hatari za uwekezaji, ili kuendelea kutunza mtaji na kupata faida za ushindani, anahitaji utaalumu, gawio, uwazi, urahisi wa kuweka na kutoa fedha zake na gharama nafuu za uendeshaji, vyote vinaweza kupatikana kwenye mifuko yetu ya uwekezaji wa pamoja."

Taasisi ya UTT AMIS ni ya kiserikali na inasimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa zaidi ya miaka 17 sasa, ikitoa fursa Watanzania kuwekeza katika mifuko yake ambayo ni; Mfuko wa Umoja, Mfuko wa Watoto, Hatifungani, Jikimu, Wekeza Maisha na Mfuko wa Ukwasi ili kutunza thamani ya fedha, kukuza mitaji yao na kupata gawio.

Mwishoni mwa mwaka jana, UTT AMIS ilifanya Mikutano Mikuu ya Mwaka ya Mifuko hiyo ya Uwekezaji, huku ikijivunia mafanikio makubwa pamoja na kuwepo changamoto ya janga la Uviko-19.

Mkurugenzi Mtendaji wa UTT AMIS, Simion Migangala, akatangaza mafanikio hayo kwa wawekezaji wa mifuko yote imefanya vizuri, kwa kuainisha: Mfuko wa Umoja thamani ya kipande imeongezeka kwa Sh. 104.0 hadi Sh. 740.0 sawa na faida ya asilimia 16.6 kwa mwaka ulioishia Juni 2021.

Anasema Mfuko wa Umoja ni wa kwanza kuanzishwa mwaka 2005 na umeendelea kufanya vizuri kwa miaka 16 mfululizo. Anaufafanua uko wazi na unawalenga wawekezaji wenye lengo la muda mrefu na kati.

Kwa sasa, UTT AMIS ina jumla ya mifuko sita ambayo ni: Umoja, Watoto, Wekeza Maisha, Kujikimu, Ukwasi na Hati Fungani.

**INAFANYAJE KAZI?**

Ofisa Masoko - Mwanga, anaielezea Nipashe namna mifuko ya UTT AMIS inavyofanya kazi huku ikiacha faida lukuki kwa mwekezaji.

Kwanza anasema, UTT AMIS imepewa leseni kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kukusanya amana kutoka kwa wawekezaji na kuziwekeza.

"Tukishapata hizo fedha tunaenda kuwekeza katika masoko ya fedha na mitaji kulingana na waraka wa toleo la mfuko. Faida inayopatikana inarejeshwa na kugawanywa kwa wawekezaji na sehemu ya uwekezaji wao katika mfuko ndio inafahamika kama kipande," anafafanua Mwanga.

Mwanga anasema masoko ya mitaji, ni fedha inayohusisha dhamana za uwekezaji zaidi ya mwaka mmoja. Anafafanua: "Mfano kuna kuwekeza kwenye Hisa ambazo zimeorodheshwa na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), pia kuna kuwekeza kwenye hati fungani za serikali za muda mrefu na hati fungani za kampuni."

**FAIDA YA KUWEKEZA**

Mwanga anasema, faida ya uwekezaji inajumuisha nafasi ya kupata faida shindani sokoni, pia hatari za uwekezaji zikipunguzwa kwa kufanya uwekezaji mseto

"Mifuko ya uwekezaji inawezesha wawekezaji wadogo kupata fursa za kuwekeza kwenye masoko ya fedha na mitaji kwa viwango vidogo vya fedha tena mara kwa mara.

"Wawekezaji, pia wanapata fursa ya kuwekeza kwenye dhamana, ambazo katika hali fulani mwekezaji mmoja mmoja inakuwa ni ngumu au ghali kuweza kupata dhamana hizo," anasema.

"Kampuni ya UTT AMIS, imekuwa ikitoa elimu ya fedha mara kwa mara kwa makundi tofauti juu ya faida na jinsi ya kuwekeza katika mifuko yao, kwa malengo ya muda mfupi hadi mrefu." anasema Mwanga

**MFUKO WA UMOJA**

Mwanga anaeleza, Mfuko wa Umoja uko wazi na wenye uwiano sawa wa uwekezaji, akiufanya kuwa bora na wenye uwekezaji wa kiwango cha kati.



Naibu Spika wa Bunge, Mussa Azzan Zungu akipewa maelezo kutoka kwa Ofisa Masoko na Uhusiano wa UTT AMIS, Dorice Mlenge, jinsi mifuko ya uwekezaji wa pamoja inavyowanufaisha machinga wakati wa maonyesho ya wamachinga yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

Pia, ni mfuko unaowekeza kiwango kisichozidi asilimia 50 ya fedha zake kwenye hisa zilizoorodheshwa DSE na asilimia 50 nyingine zinawekezwa kwenye masoko mengine ya fedha na mitaji yenye sifa tofauti.

Sera ya uwekezaji kwa upande mmoja, ni mpango uliowekwa na mfuko kutawanya rasilimali zake. Pia, ni mpango mkakati na kinga, endapo eneo moja la uwekezaji linafanya vibaya.

Aidha, anaueleza ni uwekezaji kwenye hisa ulio kwa kiwango cha chini, ikilinganishwa na eneo lenye mapato ya kudumu (fixed Income).

Mwanga anasema, thamani ya kipande kwa sasa imeongezeka kwa Sh. 104.0 na kufikia Sh. 740.0 kwa kila kipande, sawa na faida ya asilimia 16.6 kwa mwaka ulioishia Juni 2021.

Hapo anafafanua kuwa Mfuko wa Umoja ni mfuko wa kwanza kuanzishwa na UTT AMIS mwaka 2005 na umeendelea kufanya vizuri kwa muda wa miaka 16 mfululizo ambapo mfuko huo ni wa wazi ambao unalenga wawekezaji wenye lengo la muda mrefu na wa kati.

**MFUKO WA UKWASI**

Anasema, madhumuni ya mfuko huo ni mpango unaotoa njia nyingine ya uwekezaji kwa wawekezaji, wanaotaka kuweka fedha kwa kipindi cha muda mfupi na mrefu. Hatari na athari kidogo katika uwekezaji na ukwasi wa hali ya juu, ndio dhumuni hasa la mfuko huu.

Anaieleza Sera ya Uwekezaji kuwa ni kiwango cha chini cha uwekezaji katika masoko ya fedha, itakuwa asilimia 50 na fedha inayobaki itawekezwa katika Dhamana za Serikali. Huo ni mfuko usiowekeza kwenye hisa.

"Chaguo la mpango wa Uwekezaji wa Mfuko huu; unatoa fursa ya kukuza mtaji. Pia mwekezaji anaweza kutoa fedha zake wakati wowote bila gharama yoyote," anafafanua.

Nani anaruhusiwa kuwekeza? Mfuko uko wazi kwa Mtanzania aliye ndani au nje ya nchi, ikihusisha mtu binafsi (ikijumuisha watoto), asasi kama mifuko ya pensheni, benki, taasisi za serikali, vyombo vya ulinzi na usalama, asasi zisizo za kiserikali na mashirika mengineyo.

Anaeleza Mfuko wa Ukwasi, umeongezeka ukubwa kwa Sh. bilioni 103.1 sawa na asilimia 91.4; ikimaanisha kutoka Sh. bilioni 112.8 Juni, 2020 hadi shilingi bilioni 215.9 Juni 30,2021.

Mwanga anaongeza, pia katika kipindi hichohicho thamani ya kipande iliongezeka kwa shilingi 37.5 sawa na faida ya asilimia 15.3 kwa mwaka.

"Faida ya Mfuko wa Ukwasi kwa kipindi cha mwaka mmoja ni asilimia 15.3 ikilinganishwa na faida ya asilimia 15.1 ulionakiliwa mwaka uliopita 2020. Faida ya asilimia 15.3 ni tafsiri ya ongezeko kwenye mtaji wa mwekezaji aliyewekeza kwa mwaka mmoja," anasema Migangala

**MFUKO WA WATOTO**

Mwanga anaufafanua kuwa, mfuko huo ni mpango ulio wazi kwa watoto unaokusudia kukuza mtaji kwa muda mrefu kupitia uwekezaji wa mseto, kwa kuwekeza kwenye hisa zilizoorodheshwa kwenye soko la hisa na dhamana.

Umri wa mtoto wa kujiunga na mfuko, uwekezaji unafanywa kwa mtoto wa umri chini ya miaka 18 na anayeruhusiwa kuwekeza: kwa Watanzania walio ndani na nje ya nchi, pia watu binafsi, kampuni, taasisi, benki na asasi za kiraia, huku uwekezaji ukitakuwa ufanywe kwa manufaa ya mtoto.

Anaeleza, kwa kipindi Juni, 2020 hadi Juni 30,2021 thamani ya kipande iliongezeka hadi kufikia Sh. 455.2 kutoka Sh. 380.9 mwaka jana, akisema ukubwa wa mfuko huo ni Sh. bilioni 4.2, ikilinganishwa na Sh. bilioni 3.5 ya Juni 30,2020 ikiwa sawa na ongezeko la Sh. bilioni 0.7 (+20.0%).

**MFUKO WA JIKIMU**

Mwanga anasema kuwa lengo la Mfuko wa Jikimu ni kukuza na kutoa gawio kutokana na mapato ya ziada kwa vipindi tofauti, pia kumkuzia mwekezaji mtaji.

Anasema, mfuko unatoa fursa mbili za uwekezaji, mapato ya robo mwaka, pia mwaka mzima, kwa kuambatanisha na ukuaji wa vipande.

Kiwango cha chini cha uwekezaji katika mfuko huo kwa Mpango wa Mapato ya Robo Mwaka, unatajwa ni Sh. milioni 2 na Sh. milioni 1 kwa Mpango wa Gawio kwa Mwaka; pia Sh. 5,000 kwa Mpango wa Ukuaji Mtaji kwa mwaka.

"Kiwango cha chini cha uwekezaji wa nyongeza au unaofuata (additional investment) ni Sh.15,000 kwa mpango wowote wa gawio na Sh.5,000 kwa mpango wa ukuaji mtaji kwa mwaka, hakuna ukomo wa kiwango cha kuwekeza," anafafanua.

Anataja faida nyinginezo katika Mfuko wa Jikimu kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2021, ulilipa gawio lenye thamani ya shilingi bilioni 1.2 au sawa na Sh. 12.0 kwa kila kipande.

"Hadi kufikia Juni 30,2021 rasilimali za mfuko zilifika shilingi bilioni 17.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 17.6 mwaka uliopita," anasema na kuongeza kuwa;

"Faida ya Mfuko wa Jikimu iliendelea kuimarika na kuongezeka kutoka asilimia 15.6 katika mwaka wa fedha uliopita (2019/2020) hadi asilimia a18.8 katika mwaka wa fedha ulioisha Juni 30,2021."

**HATI FUNGANI**

Mwanga anaeleza Mfuko wa Hatifungani kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30,2021 faida ilikuwa asilimia 15.7 ikilinganishwa na asilimia 16.2 mwaka uliotangulia.

"Mfuko wa Hati Fungani umelipa gawio la shilingi 1.0 kila mwezi sawa na shilingi 12.0 kwa muda wa mwaka mmoja," anasema

**MFUKO WEKEZA**

Mwanga anautaja kuwa Mfuko Wekeza Maisha, una zaidi ya miaka 10 sasa, ukiambatanishwa na faida za bima. Mwekezaji katika mfuko huo, ana lengo la kiasi anachotaka kuwekeza katika muda wa miaka 10, kiwango cha chini ni Sh. milioni moja. Ni hiari yake kuwekeza kwa mkupuo au awamu.

"Mtu ukichagua kuwekeza kiasi hicho (Sh. milioni moja) kila mwezi atahitajika kuwekeza kiasi cha Sh. 8,340 tu ili kukamilisha mpango wake wa uwekezaji.

"Zaidi ya asilimia 99 ya fedha za mwekezaji huwekezwa na chini ya asilimia moja hutumika kugharamia bima," anasimulia, akitaja aina ya bima hizo ni za maisha, ulemavu wa kudumu na ajali.

Mwanga anatoa mfano binafsi, baada ya miaka 10 alifungua kiwanda kidogo cha kutotoa mayai ya kuku na kuuza vifaranga na mayai, akifafanua: "Niliweza kununua mashine (incubator) kwa sasa kipato changu kimeongezeka sana."

Mwanga anakumbusha ukubwa wa mfuko huo kwa sasa umeongezeka kwa Sh. milioni 400 (ziada 28.6%) hadi shilingi bilioni 1.8 kutoka shilingi bilioni 1.4 mwaka 2020.

"Thamani ya kipande kwa muda wa mwaka mmoja ulioishia Juni 30,2021 iliongezeka kwa shilingi 125.8 (25.6%) hadi kufikia shilingi 617.3 kwa kila mwaka." anasema

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Hivi kweli Uviko-19 unaishi kwa adabu?






NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

WAKATI bado naishi kijijini, Madongoporomoka, kulikuwa na jipaka fulani hivi jeusi, lakini jizi kwapukwapu sana, likikwapua kila kitu mbele yake na hususan kitoweo.

Liliweza hata kusukuma mlango uliosindikwa kizembe na kuondoka na lilichokikuta humo ndani. Hakika lilisumbua sana, licha ya kuwindwa, lakini lilikwepa mitego mbalimbali.

Hata hivyo, ilifika wakati likapata kichapo cha nguvu na kuonekana kushika adabu na ndipo tulipoweza kukaa sawa na kupumzika, kwani lilionekana hata kushika adabu na kunywea.

Ilifika wakati likajikausha na hata baadhi ya milango ilipoachwa wazi lilishindwa kuingia kwa kuchekea kichapo na badala yake kubaki kutupiwa mifupa na mabaki ya chakula, likakonda.

Tulijisahau tukadhani limeshika adabu, lakini kumbe wanyama nao wana akili zao, lilikuwa linatuvizia tujisahau, likaanza kukwapua tena safari hii likawa linapora hata watoto wadogo samaki viganjani.

Tulijilaumu sana kujisahau, lakini tukachelewa kulidhibiti tena, ingawa lilikufa kwa uzee, lakini likabakiza mbegu zake, kwani lilikuwa limezaa na wanawe waliokuwa kijijini hapo na bila shaka mtoto wa paka ni paka tu.

Walioko kijijini bado wananiambia wajukuu wa huyo paka wapo na wanaonyesha tabia ileile, ingawa si kwa kasi ya nyanya yao huyo, lakini wanasumbua hapa na pale katika masuala ya ukwapuaji. Nimeikumbuka hii kutokana na sisi Wabongo kujisahaulisha mambo na kuona yako sawa, kumbe jipaka linapiga mahesabu yake kimya kimya na ipo siku likiibuka litafanya ya kufanywa na kutuacha vinywa wazi.

Hivi nani kasema Uviko-19 imetoweka? Nani katuambia Uviko-19 inaishi kwa adabu kama alivyopata kujigamba mzito fulani alikokuwa kileleni katika chama kikubwa kitaifa? Tunajisahaulisha kumbe eh!

Nakumbuka miaka ya 2019 na 2020 tulipohaha baada ya corona kuingia nchini na kutupukuchua kama mahindi kwenye gunzi.

Tulihaha tukivutana kwenye barakoa, huku tukiendelea kupukutika, kana kwamba hatukuwa na akili zinazoendana!

Mnakumbuka ilipofikia kuwahi kutolewa kauli kwao wabunge wa nje ya jiji wasionekane Dar es Salaam, eti warudi wanakotakiwa, kwa sababu wanaleta Uviko-19 jijini! Tunajiaminisha hivi sasa kwamba Uviko-19 haipo kwa mfano wetu wa bibi paka ameshakufa na kudhani kafa na wanawe, pia wajukuu zake! Tunajidanganya mchana kweupe Watanzania, lakini tujue likiibuka tena, tujiandae.

Tunashuhudia sasa mikusanyiko kama kawa, tunakusanyika viwanjani kushuhudia mechi, tunakusanyika kuzika, tunakusanyika maandamano, tunakusanyika kusherehekea harusi na kadhalika, bila kinga bila uoga.

Tumerudi kwenye hulka ileule ya kuvaa barakoa tunapomuona mkuu wetu kava. Nakumbuka siku moja kigogo mmoja mheshimika kabisa, tena akiwa kwenye jengo la imani amevaa barakoa, alipoingia mkuu wake bila ya barakoa, naye akavua ya kwake.

Nilishangaa na kujiuliza kama huyo mkuu alikuwa anaishi kwa niaba ya huyo kigogo. Maisha ni yako, lakini unashindwa kuyatetea mpaka uone fulani anatetea yake, ndipo nawe uige?

Tunashuhudia baadhi wenye dhamana ya kupambana na Uviko-19 hawasemi sana ya ugonjwa huo, kana kwamba haupo tena. Tumetawaliwa na mengine kabisa na sasa kujadili vita vya Russia na Ukraine na kusahau vita vya Uviko. Kweli?

Hivi kwa kujiaminisha hivi, tunaamini wimbi lingine jipya likivamia tutabaki salama kweli? Tutabaki tunashinikiza malalamiko tu kwamba tuna Ukraine, mafuta yamepanda na sasa Uviko nyingine imerudi na kubaki kumlaumu Mungu.

Kinachoonekana hapa hivi sasa utadhani Uviko-19 inalenga kumwambukiza Chifu Hangaya na wasaidizi wake tu, kwani ndio mimi nawaona wanajali barakoa kuliko wengine, huku tulivizia tukiwa naye karibu nasi tunadiriki kuvaa.

Nilishangaa hivi karibuni Arusha kwenye mkutano wa Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani, alipokuja mkuu, ndipo tukatangaziwa kuvaa barakoa, ina maana bila yeye tusingevaa! Haya tusubiriane tu tutakujaumbuka! Alamsiki!

UCHUMI

TARI RASMI YAGONGA HODI...

# Kung'ara kwa walima tangawizi kitaifa Same na magonjwa 'yanawavuta shati'

**Na Ashton Balaigwa, SAME**

TANGAWIZI ni zao la viungo nchini linalostawi milimani na baadhi ukanda wa tambarare, maeneo ya kitropiki kutoka usawa wa bahari, mwinuko wa mita 1500 au zaidi na inahitaji mvua kiasi cha milimita 1200 hadi 1800 na joto sentigredi 20 hadi 25, lenye udongo tifutifu, rutuba na isiotuamisha maji.

Hapo kunapatikana mikoa ya Kilimanjaro wilayani Same, Mbeya, Ruvuma, Morogoro, Kigoma ,Pwani, Kagera, pia visiwani Zanzibar.

Tangawizi ni kiungo kinachoongeza ladha na harufu katika vinywaji kama juisi, pia vyakula nyama, mikate, biskuti na keki. Pia, ni muhimu katika utengenezaji dawa kama za mafua,kikohozi na pumu,

Umaarufu wake umeongezeka karibuni kutokana na mlipuko wa ugonjwa Covid 19, tangawizi imetumika katika dawa mbalimbali kutibu au kinga dhidi ya maradhi hayo.

MAMBO YA SAME

Wilaya ya Same ina historia ya kuongoza kilimo cha tangawizi, kuanzia kata ya Miamba tangu mwanzoni mwa miaka 1990 na baadae kuenea katika kata nyingine tisa, ambako kilimo hicho kimeshamiri.

Mwenyekiti wa Ushirika wa Wakulima wa Tangawizi, Mbaraka Ally,anasema kuongezeka uzalishaji unaofikia zaidi ya tani 25,000 kila msimu, umeshinikiza kuanzishwa kiwanda cha kusindika tangawizi kikubwa zaidi Ukanda wa Afrika Mashariki.

Ghafla kuanzia mwaka 2018, uzalishaji tangawizi ulianza kukumbwa na changamoto ya mlipuko wa magonjwa kama kuoza matunguu na madoa kwenye majani yanayobadilika rangi kuwa njano.

Hapo ikachangia uzalishaji kushuka kwa kasi kutoka wastani tani 25 hadi 30 kwa ekari, kuteremka kuwa tani 10 hadi 15.

Hilo likamuibua aliyekuwa Naibu Waziri wa Kilimo (sasa Waziri) Hussein Bashe, mnamo Julai 18 hadi 9 mwaka jana, akafanya ziara wilayani Same alikopokea malalamiko ya wakulima katika kata ya Miamba, kuhusu kuwapo magonjwa yanayoozesha tangawizi.

Pia walimueleza Waziri Bashe namna kipato chai kinashuka, wakiomba serikali kupitia Wizara ya Kilimo kuingilia kati.

**ALICHOKIFANYA BASHE**

Baada ya kusikiliza kero hizo,Waziri Bashe aliagiza Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania(TARI) kupeleka wataalamu wa magonjwa ya mimea kutafiti kinachoathiri tangawizi na kuwapa majibu wakulima, watatue tatizo hilo.



Mkurugenzi wa Utafiti na Ubunifu kutoka TARI Makao Makuu, Dk Joel Meliyo (wa pili kutoka kushoto),akitoa elimu kwa wakulima kuhusu magonjwa yanayoshambulia tangawizi katika kata ya Miamba wilaya Same mkoani Kilimanjaro. **PICHA: ASHTON BALAIGWA.**

Aidha, akiagiza TARI kuanzisha Kitalu cha kuzalisha mbegu za tangawizi kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Same, huku uongozi wa wilaya ukipewa maelekezo kutenga eneo la kuikabidhi TARI, ambako kungetumika kuzalisha mbegu kwenye kata ya Miamba.

**UTEKELEZAJI ULIVYO**

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk Geoffrey Mkamilo,anasema wakapokea na kutekeleza agizo la Waziri Bashe haraka, kwa kupeleka timu ya watafiti kutoka kituo cha Tengeru, Arusha na walianza kazi kwenye mashamba ya wakulima, walikochukua sampuli za udongo na majani ya zao hilo.

Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti cha TARI -Tengeru,Mpoki Shimwela, anafafanua malengo mahususi yalikuwa kutambua aina ya magonjwa kwa kutembelea maeneo yaliyoathirika, pia kutoa ushauri wa namna bora ya kudhibiti magonjwa.

Anasema, walijikita katika aina ya vimelea vinavyosababisha magonjwa hayo, namna ya kuyadhibiti na kupunguza kusambaa ugonjwa wa kuoza na kukauka majani katika maeneo mengine kunakolimwa tangawizi.

**MATOKEO YA UTAFITI.**

Akiwasilisha matokeo ya utafiti huo kwa wakulima na Mkuu wa Wilaya ya Same, Edward Mpogolo, Mkurugenzi wa Utafiti na Ubunifu kutoka TARI Makao Makuu,Dk. Joel Meliyo, anasema wamebaini kuwepo magonjwa yanayosababishwa na bakteria, pia fangasi, tatizo kuu ni kuwepo mbegu zisizo za uhakika zinazowezesha kubeba magonjwa, pia kupungua rutuba udongo.

Anafafanua, kubainika kilimo duni cha tangawizi na kutokuwapo chanzo salama cha uzalishaji au uhakika wa mbegu, wakulima wengi wakiandaa mbegu kienyeji.

Dk. Mileryo anasema wakulima wanatumia mbolea ya samadi zenye walakini wanazonunua kutoka kwa wafugaji, kunakonyeshewa mvua, pia kukaa juani muda mrefu, kunapoteza virutubisho.

Anataja wamebaini magonjwa na dalili za upungufu mkubwa wa virutubisho, akivitaja kwa majina ya kitaalamu 'Potassium' na 'Naitrojeni' katika maeneo mengi ya uzalishaji.

Bosi huyo wa utafiti wa TARI, anasema wamebaini dalili za madoa katika majani zikiashiria kuwepo magonjwa yanayosababishwa na viini vya ugonjwa uitwao 'Phyllosticta Zingiber'akifafanua dalili zake za madoa.

Dk. Meliyo anasema, kutokana na utafiti huo, wamewashauri wakulima wengi kusafisha mashamba, kuepuka umwagiliaji kwa njia ya anayoiita 'sprinkier' inayoeneza magonjwa na kufanya kilimo cha mzunguko kwa maeneo yaliyoathirika, wakipanda mazao mengine yasiyokuwa katika kundi moja na mimea iliyoathirika.

Ushauri mwingine anautaja, wakulima watumie mbolea za viwandani na samadi, wakifuata kiwango kinachoshauriwa kila mwaka cha 'Naitrojeni' na 'Pottasium' kwa kuwa tangawizi asili yake ni zao la mizizi, lipandwe kwa mstari kuwezesha kufanyika palizi na kunyanyua udongo.

**AHADI YA TARI**

Mratibu wa Taifa wa Usambazaji wa Teknolojia za Utafiti za Kilimo kutoka TARI Makao Makuu, Mshaghuley Ishika, anasema baada ya kubaini magumu ya wakulima, wanakusudia kuweka kambi katika vijiji hivyo kunakolimwa tangawizi wawaelimishe.

Ishika anadokeza wanayokusudia kuelimisha, ni namna ya kujua mbinu bora za ulimaji tangawizi, kuwasaidia, kujua matumizi bora ya mbolea na viuatilifu, muda sahihi wa kuvuna, kutengeneza mbolea ya mboji, badala ya samadi iliyo duni.

**WAKULIMA WALIVYOPOKEA**

Mkulima wa tangawizi kutoka kijiji cha Goha, William Kilango, anakiri wanafanya kilimo hicho bila ya kufuata kanuni bora, hata kusababisha kuangukia magumu ya magonjwa yanayoathiri zao hilo.

Hapo anaiomba TARI kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya Same, ipige kambi katika vijiji vyao wakiwaelimisha kilimo bora, ili iwafikie kwenye tija itakayoinua kipato chao.

Mkulima Kunt Mjema kutoka kata ya Miamba, ombi lake serikalini, waharakishiwe wataalamu kwa kuwa wameshaanza kutayarisha mashamba yao ya tangawizi.

Mkuu wa Wilaya ya Same Edward Mpogolo, anaipongeza TARI kuitikia haraka agizo la Waziri wa Kilimo, hata kufanikisha utafiti unaoondoa changamoto za walima tangawizi, akitaja inachangia asilimia 60 ya mapato ya wilaya.

## Waliokabiliwa na adha zote za umasikini na makazi, wazawadiwa nyumba mpya

INATOKA UK.11

kutafuta chakula ambapo tulijiwekea utamaduni wa kupeleka mara kwa mara.

"Nilimuunganisha na shirika letu kwenye mradi wake wa ujenzi wa nyumba kwa wajane na yatima, ingawa wakati huo kulikuwa na tatizo la Uviko 19. Kwa hiyo, mradi ulikuwa umesimama kidogo, ila jina lake lilichukuliwa na kusubiria," anasimulia.

**FUNDI MJENZI**

Fundi mjenzi, Samson Masuki, anasema amejenga nyumba hiyo kwa takribani mwezi mmoja usiku na mchana kutokana na uhalisia walioshuhudia, kutoka hali ya mama huyo.

"Alipokuja kuitazama nyumba ikiwa katika rinta, presha ilipanda na akazimia, tulipata kazi tena ya kumsaidia na baadaye kumpeleka alipokuwa akiishi, akiwa katika hali ya ugonjwa kwa kuwa hakuamini kama siku moja ninaweza kumiliki nyumba," anasimulia.

Mkurugenzi wa Shirika la Tanzania Women Reseach Foundation (TAWREF), Dafrosa Itemba, anasema lengo la mradi ni kuwapatia wanajamii maisha bora, hasa yatima na wenye ulemavu.

Anasema ili kumjengea mhitaji nyumba, ni lazima shirika lihakikishe uhalali wa kiwanja, kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, hiyo ni nyumba ya 138 tangu mwaka 2012 wamezijenga katika wilaya nne za mkoa wa Kilimanjaro, akiorodhesha; Manispaa ya Moshi nyumba 16, Halmashauri ya Moshi ziko 82, wilaya za Siha tatu na Hai 34.

Anasema ujenzi wa nyumba hiyo umegharimu Sh. milioni 10, huku wakiwa na matumaini watoto wanapokuwa wataweza kuongeza vyumba vingine na kuweka umeme.

**ALIYETOA KIWANJA**

John Malisa, ndiye ametoa eneo hilo kwa familia wahitaji, akifafanua mama huyo kupitia mkwewe Mzee Malisa.

"Baada ya kumuona mama huyu anateseka na watoto, tuliamua mimi na familia yangu kumgawia kidogo tulicho nacho ili aweze kuishi na familia yake.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

# HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI MHE. JUMAA AWESO (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23



*Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizindua mradi wa maji wa Misungwi*

# HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI MHE. JUMAA HAMIDU AWESO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

**Siku ya Alhamisi tarehe 12 Mei, 2022, Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Hamidu Aweso (Mb), aliwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka 2022/2023. Hotuba hii ina maeneo makuu manne, ambayo ni Hali ya Sekta ya Maji nchini; Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22 na Mpango na Bajeti ya Sekta kwa mwaka 2022/23; pamoja na Changamoto na Hatua zilizochukuliwa. Hapa chini ni muhtasari wa hotuba hiyo. Hotuba kamili inapatikana katika tovuti ya wizara www.maji.go.tz.**

**1.0 HALI YA SEKTA YA MAJI NCHINI**

**1.1 Rasilimali za Maji**

1. Rasilimali za maji zilizopo nchini zinakadiriwa kuwa mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka ambapo rasilimali za maji juu ya ardhi ni mita za ujazo bilioni 105 na zilizopo ardhini ni mita za ujazo bilioni 21. Hadi Aprili 2022, mahitaji ya maji kwa matumizi mbalimbali nchini yanakadiriwa kuwa ni takribani mita za ujazo bilioni 47 kwa mwaka sawa na asilimia 37.37 ya maji yaliyopo nchini. Mahitaji ya maji yanatarajiwa kuongezeka hadi wastani wa mita za ujazo bilioni 80 kwa mwaka ifikapo mwaka 2035.

2. Kiwango cha maji kilichopo kwa kila mtu kwa mwaka ni takribani wastani wa mita za ujazo 2,250 kwa kuzingatia makadirio ya idadi ya watu milioni 55.9 kwa mwaka 2019. Kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa ni wastani wa mita za ujazo 1,700 ambapo chini ya hapo nchi inahesabika kuwa na uhaba wa maji (Water Stress). Hivyo, kiasi cha maji kilichopo nchini kinaonesha kuwa nchi yetu haina uhaba wa maji.

**1.2 Ubora wa Maji**

3. Wizara kupitia maabara 17 za ubora wa maji nchini imeendelea kuhakiki na kufuatilia ubora wa maji katika vyanzo vya maji na mitandao ya kusambaza maji mijini na vijijini kwa lengo la kutoa maamuzi juu ya matumizi yaliyokusudiwa.

4. Maji yanayosambazwa kwa jamii kupitia mifumo ya usambazaji maji mijini na vijijini yameendelea kukidhi viwango vya ubora wa maji ya kunywa vya kitaifa katika maeneo mengi nchini. Hata hivyo changamoto iliyopo ni uwepo wa madini ya chumvichumvi katika maeneo ya Pwani na Ukanda wa Kati; na uwepo wa madini ya Fluoride katika maeneo yaliyopo kwenye ukanda unaopitiwa na Bonde la Ufa. Kukabiliana na changamoto za ubora wa maji, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuwekeza katika teknolojia mbalimbali za kusafisha na kutibu maji.

**1.3 Upatikanaji wa Huduma ya Maji Vijijini**

5. Hadi kufikia Aprili 2022, upatikanaji wa huduma ya maji vijijini imefikia wastani wa asilimia 74.5 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 72.3 mwezi Machi, 2021. Kiwango hicho kinatokana na kukamilika kwa ujenzi wa miradi mipya, ukarabati na upanuzi wa miradi 301 ambayo imeanza kutoa huduma kwa zaidi ya wananchi 1,336,860.

**1.4 Upatikanaji wa Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini**

6. Hadi kufikia Aprili, 2022 hali ya upatikanaji wa huduma ya maji mijini ni wastani wa asilimia 86.5 ikilinganishwa na asilimia 86 ya Machi 2021. Ongezeko hilo linatokana na kukamilika kwa ujenzi wa miradi 40 iliyohusisha ukarabati, upanuzi na ujenzi wa miradi mipya.

7. Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji inatarajiwa kuongezeka ifikapo mwezi Desemba 2022 kutokana na miradi mikubwa ya maji inayotarajiwa kukamilika ndani ya kipindi hicho ikiwemo mradi wa kuboresha huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Arusha; Mradi wa Maji wa Mugango-Kiabakari- Butiama; Mradi wa kupeleka maji kwenda Miji ya Tinde – Shelui; Mradi wa maji Kigamboni; Bunda; Chalinze; Kyaka-Bunazi; Namanga; Bagamoyo; pamoja na miradi 218 inayotekelezwa kwa fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19 maeneo ya vijijini na mijini.

**2.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2021/22**

**2.1 Upatikanaji wa Fedha**

8. Mwaka 2021/2022, Wizara ya Maji iliidhinishiwa jumla ya Shilingi bilioni 680.39 na kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 33.76 zilikuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 646.63 zilikuwa ni fedha za maendeleo. Aidha, wakati bajeti inaendelea kutekelezwa, Wizara ilipata Shilingi bilioni 139.35 kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO - 19 ili kuhakikisha wananchi wanapata majisafi, salama na yenye kutosheleza karibu na makazi yao na kuwezesha kupambana na UVIKO-19. Hatua hiyo, imewezesha bajeti ya maendeleo kuongezeka na kuwa Shilingi bilioni 785.98 na jumla ya bajeti yote kwa mwaka 2021/2022 kufikia Shilingi bilioni 819.74.

9. Hadi Aprili 2022, Wizara imepokea jumla ya Shilingi bilioni 778.91 sawa na asilimia 95 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, Shilingi bilioni 743.76 ni za kutekeleza miradi ya maendeleo sawa na asilimia 94.6 ya bajeti ya fedha za maendeleo. Kwa upande wa fedha za Matumizi ya Kawaida, jumla ya Shilingi bilioni 35.15 zilipokelewa sawa na asilimia 104 ya bajeti ya fedha za Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 22.61 ni fedha za mishahara (PE) na Shilingi bilioni 12.54 ni fedha za matumizi mengineyo (OC).

**2.2 Programu na Miradi Mbalimbali Iliyotekelezwa katika mwaka 2021/22**

10. Hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa baadhi ya miradi na mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:-

**3.2.1 Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji**

11. Hadi Aprili 2022, jumla ya vituo 178 vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji vimejengwa na kukarabatiwa; vimetolewa vibali vipya 451 vya matumizi ya maji; vibali 649 vya kuchimba visima vya maji; pamoja na kuweka mipaka vyanzo vya maji 48 kama hatua ya awali ya uhifadhi.

**3.2.2 Huduma za Ubora wa Maji**

12. Katika mwaka 2021/22, kupitia Maabara za Ubora wa Maji Wizara imeendelea kusimamia na kufuatilia ubora wa maji kwa kukusanya na kuchunguza sampuli kutoka katika mifumo ya usambazaji maji kwa matumizi ya majumbani, maji katika vyanzo na maji kwa matumizi mengine ikiwa ni pamoja na viwanda, umwagiliaji, ujenzi, utafiti na ufugaji wa samaki. Vilevile, Wizara imeendelea kuhakiki na kufuatilia ubora wa madawa ya kusafisha na kutibu maji pamoja na kuhakiki ubora wa majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira. Aidha, katika kulinda afya za wananchi katika mikoa iliyoathirika zaidi na madini ya Fluoride, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Uondoaji wa Madini hayo kwenye maji ya kunywa na kupikia.

**3.2.3 Huduma za Usambazaji Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini**

13. Katika mwaka 2021/22, Serikali kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ilipanga kujenga, kukarabati na kufanya upanuzi wa miundombinu ya maji katika miradi 1,176. Hadi Aprili 2022, ujenzi na ukarabati wa miradi 301 umekamilika na kuanza kutoa huduma ya majisafi na salama. Ujenzi na ukarabati wa miradi 52 unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2022 na utekelezaji wa miradi 823 utaendelea katika mwaka 2022/23.

**Utekelezaji wa Miradi yenye Changamoto za Muda Mrefu**

14. Wizara kupitia RUWASA imeendelea kukwamua miradi yenye changamoto za muda mrefu ambapo katika mwaka 2021/22, jumla ya miradi 42 imekamilishwa na kuanza kutoa huduma kwa wananchi na hivyo kufikisha miradi 127 kati ya miradi 177.

**Uimarishaji wa Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii**

15. Kwa muda mrefu miradi ya maji vijijini iliyokamilika katika baadhi ya maeneo imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya kutokuwa endelevu. Serikali kupitia Sheria Na. 5 ya Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019 ilifanya maboresho ya muundo wa Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs) ambapo muundo wa sasa unajumuisha wataalam wakiwemo Mafundi Sanifu wanaosimamia matengenezo ya miundombinu na Wahasibu wanaosimamia masuala ya fedha. Aidha, CBWSOs 2,466 zimeundwa na kuhuishwa hadi sasa. Vilevile, CBWSOs zimeajiri jumla ya wataalam 1,746 kwa mikataba ambapo kati yao Mafundi Sanifu ni 940 na Wahasibu 806.

**3.2.4 Huduma za Usambazaji wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini**

16. Katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya miradi 114 ilipangwa kutekelezwa katika maeneo ya mijini ambapo hadi Aprili 2022, jumla ya miradi 40 imekamilika na kuanza kutoa huduma. Aidha, utekelezaji wa miradi mingine unaendelea ikiwemo:-

**Miradi ya Kuboresha Huduma ya Maji katika Jiji la Dodoma**

17. Serikali imeendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Dodoma ambapo Wizara imekamilisha utekelezaji wa miradi ya kutoa maji katika visima vya Ihumwa kwenda tanki la Njedengwa; mradi wa kuboresha hali ya upatikanaji wa majisafi Chamwino – Ikulu. Aidha, Wizara inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kuchimba visima vipya na kukarabati visima vya zamani.

18. Katika jitihada za kukabiliana na uhaba wa huduma ya maji katika jiji la Dodoma, Serikali imepata mkopo wa Dola za Marekani milioni 125.3 kutoka Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Bwawa la Farkwa na mtambo wa kutibu maji ambapo ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2022/23.

**Miradi ya Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya Maeneo ya Mkoa wa Pwani**

19. Serikali imekamilisha utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma ya maji wa Mlandizi – Chalinze – Mboga kwa gharama ya Shilingi bilioni 18. Mradi huo ulizinduliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Machi 2022. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inaendelea na ukarabati na upanuzi wa mfumo wa usambazaji majisafi kutoka kwenye tanki la Chuo Kikuu cha Ardhi kwenda Bagamoyo ambapo utekelezaji umefikia asilimia 61. Vilevile, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa kusambaza maji katika maeneo ya Mbezi-Makabe ambapo utekelezaji umefikia asilimia 70.

**Mradi wa Maji Mugango – Kiabakari - Butiama**

20. Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA) na Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (Saudi Fund for Development – SFD) inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji wa Mugango, Kiabakari na Butiama ambao umefikia asilimia 54.

**Mradi wa maji Tinde - Shelui**

21. Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India kupitia Benki ya Exim-India inatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika miji ya Tinde na Shelui ambao umefikia asilimia 60.7.

**Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Miji 28**

22. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya India kupitia Benki ya Exim - India inategemea kuanza ujenzi wa mradi wa kuboresha huduma ya maji katika miji 28 ya Tanzania Bara na mji mmoja visiwani Zanzibar kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 500. Hadi Aprili 2022, taratibu za kuwapata wakandarasi wa ujenzi katika miji 24 zimekamilika ambapo ujenzi wa miradi katika miji hiyo itatumia fedha za mkopo wa India na miji minne (4) ya Mafinga, Makonde, Songea na Tarime-Ryorya utekelezaji wake utafanywa kwa kutumia fedha za ndani. Mikataba ya ujenzi kwa miji 24 inatarajiwa kusainiwa kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2021/22.

**Miradi ya Maji katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa**

23. Serikali imeamua kutumia vyanzo vya uhakika vikiwemo maziwa makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa kupeleka maji katika mikoa ya Mwanza, Geita, Simiyu, Kagera, Mara, Katavi, Kigoma na

# HOTUBA WIZARA YA MAJI

Rukwa, Ruvuma na Njombe.

**Miradi Mingine Inayotekelezwa**

24. Miradi mingine inayoendelea na utekelezaji ni pamoja na mradi wa kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira Arusha; Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Kigoma; Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Lindi; Mradi wa Kuboresha Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Morogoro; mradi wa maji kutoka Mto Kiwira hadi Jiji la Mbeya; mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika Jiji la Tanga; mradi wa maji Dareda-Singu-Sigino-Bagara; mradi wa majisafi wa Kyaka – Bunazi; Mradi wa Maji Same – Mwanga – Korogwe; Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Mkoa wa Simiyu; pamoja na miradi inayotekelezwa kwa kutumia fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19.

**3.2.5 Miradi ya Usafi wa Mazingira**

25. Serikali imeendelea kuboresha huduma ya usafi wa mazingira kwa kujenga, kupanua na kukarabati miundombinu ya majitaka katika maeneo mbalimbali ya mijini. Hadi Aprili 2022, hali ya uondoshaji majitaka imefikia asilimia 13.5. Lengo ni kufikia asilimia 30 mwaka 2025.

26. Upande wa vijijini, Serikali imeendelea kutekeleza Kampeni ya Usafi wa Mazingira kwa lengo la kuboresha huduma ya usafi wa mazingira katika maeneo ya vijijini. Kupitia Kampeni hiyo, Wizara imekamilisha miradi 137 ya usafi wa mazingira katika vituo vya kutolea huduma za afya na shule na inaendelea na utekelezaji wa miradi 276.

**3.0 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA**

27. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi 2022, Sekta ya Maji imeendelea kufanya maboresho ya kiutendaji na kitaasisi ambayo yameleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara na miradi mbalimbali. Kuimarika kwa ufanisi huo katika Sekta ya Maji kumeleta mafanikio yakiwemo:-

(i). Kuongezeka kwa upatikanaji wa fedha za bajeti za kutekeleza miradi ya maji vijijini na mijini kutoka shilingi bilioni 396.77 sawa na asilimia 54.1 mwezi Aprili 2021 hadi shilingi bilioni 778.92 sawa na asilimia 95 mwezi Aprili 2022;
(ii). Kukamilika na kuanza kutoa huduma kwa miradi 127 kati ya 177 iliyokuwa na changamoto za muda mrefu;
(iii). Kununuliwa kwa seti 25 za mitambo ya kuchimba visima, seti 5 za ujenzi wa mabwawa na seti 4 za vifaa vya utafiti wa maji chini ya ardhi;
(iv). Miradi kukamilika kwa wakati baada ya kuchukuliwa hatua stahiki kwa wakandarasi na wataalam wasiowajibika;
(v). Kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa huduma za maji nchini kutoka asilimia 72.3 vijijini na 86 mijini mwaka 2020/21 hadi asilimia 74.5 vijijini na 86.5 mijijni;
(vi). Kukamilika kwa jumla ya miradi 341 ya maji, kati ya hiyo ya vijijini ni miradi 301 na mijini miradi 40. Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na Misungwi (Mwanza), Orkesumet (Simanjiro), Chalinze-Mboga (Pwani) na Longido (Arusha);
(vii). Kukamilika na kuanza kutumika kwa mfumo wa taarifa za miradi na huduma ya maji ambao utakuwa ukipatikana kupitia simu za kiganjani unaojulikana kwa jina la Maji Mobile Application (Maji_App). Mfumo huo umerahisisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za miradi ya maji pamoja na hali ya huduma ya maji nchini;
(viii). Kukamilika na kuanza kutumika mfumo wa pamoja wa Uandaaji wa Ankara za Malipo ya Maji (Unified Billing System) unaosaidia kupunguza malalamiko ya ankara za maji kwa wateja; na
(ix). Kuimarika kwa usimamizi wa rasilimali za maji kwa kuendelea kutambua, kuweka mipaka na kuhifadhi vyanzo 178 vya maji pamoja na kuandaliwa kwa mipango ya utunzaji wa maeneo ya vidakio vya maji katika mabonde yote nchini.

**4.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZINAZOCHUKULIWA**

28. Katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2021/22, Wizara imekabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya uwekezaji wa miradi mikubwa ya maji; uchelewaji wa upatikanaji wa misamaha ya kodi kunakosabisha kuchelewa kukamilika kwa miradi ya maji; upungufu wa watalaam katika Sekta ya maji; na mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha mafuriko na ukame katika vyanzo vya maji kwa mfano mwaka 2021, katika kipindi cha kiangazi Mto Ruvu ulipungua kina na kuathiri upatikanaji wa maji katika Mkoa wa Dar es Salaam na hivyo kulazima hatua za dharura kuchukuliwa na Serikali.

29. Hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa kukabiliana na changamoto, ikiwemo kuendelea kutafuta vyanzo vya fedha ikiwa ni pamoja na kutumia fedha za ndani kutekeleza miradi mikubwa; kutoa elimu kwa wananchi kulinda miundombinu ya maji pamoja na kutoa adhabu kali kwa wezi wa maji na wahujumu wa miundombinu ya maji; kuongeza kasi ya ufuatiliaji wa misamaha ya kodi; kutenga na kuajiri watalaam wa kutosha; pamoja na kutekeleza mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kutekeleza miradi ya maji ambayo itatumia vyanzo vya maji vya uhakika kama vile mito mikubwa na maziwa

**5.0 VIPAUMBELE NA MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2022/23**

**5.1 Vipumbele vya mwaka 2022/23**

30. Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2022/23 ni pamoja na;
i. Kukamilisha ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miradi inayoendelea kutekelezwa;
ii. Kuanza ujenzi wa mabwawa ya kimkakati ya Kidunda na Farkwa;
iii. Kuanza ujenzi wa miradi ya maji mipya ikiwemo miradi ya maji katika miji 28;
iv. Kuendelea na shughuli za utunzaji wa vyanzo vya maji ikihusisha kutambua, kuweka mipaka na kutangaza kwenye Gazeti la Serikali ili vyanzo hivyo vilindwe kisheria;
v. Kutekeleza miradi ya maji kwa kutumia vyanzo vya uhakika ikiwemo maziwa makuu na mito mikubwa;

**5.2 Mpango wa Utekelezaji kwa Mwaka 2022/23**

**5.2.1 Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za maji**

31. Vyanzo vya maji vina mchango mkubwa katika uwepo wa rasilimali za maji na usalama wa maji kwa ujumla. Katika mwaka 2022/23, Wizara imepanga kutambua, kuweka mipaka na kutangaza vyanzo 44 kwenye Gazeti la Serikali kwa lengo la kuhifadhi na kuvilinda vyanzo hivyo kisheria; na kutekeleza Mipango ya Utunzaji wa Vidakio vya Maji iliyoandaliwa katika mabonde yote tisa nchini.

**5.2.2 Ujenzi wa Mabwawa**

32. Mradi wa bwawa la Kidunda limechukua muda mrefu kuanza ujenzi. Kutokana na azma ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ametoa kibali cha kuanza ujenzi wa bwawa hilo katika mwaka 2022/23. Aidha, Serikali itaanza ujenzi wa bwawa la Farkwa na mtambo wa kutibu maji baada ya kupata fedha za mkopo kiasi cha dola za kimarekani milioni 125.3 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Hii inaonesha nia njema ya Mheshimiwa Rais ya kumtua mama ndoo kichwani.

**5.2.3 Usimamizi wa Huduma ya Ubora wa Maji**

33. Wizara itaendelea kuimarisha uhakiki na ufuatiliaji wa ubora wa maji katika vyanzo na mifumo ya usambazaji kwa kukusanya na kuchunguza sampuli za maji na majitaka; kuhakiki ubora wa madawa ya kutibu maji kabla ya manunuzi na wakati wa matumizi; na kuendelea kuimarisha maabara za ubora wa maji kwa kuzipatia vitendea kazi, kujenga na kukarabati majengo; pamoja na kuziwezesha maabara nne (4) kupata ithibati.

**5.2.4 Huduma ya Majisafi na usafi wa Mazingira Vijijini**

34. Wizara imepanga kutekeleza jumla ya miradi 1108 ya maji vijijini ambapo miradi 672 ni miradi inayoendelea kutekelezwa na miradi 436 ni mipya. Aidha, katika kuimarisha uendelevu wa huduma za maji na usafi wa mazingira katika maeneo ya vijijini, Serikali imepanga kuzijengea uwezo CBWSOs 2,466 zilizopo na kusajili CBWSOs mpya 704.

**5.2.5 Mpango wa Matumizi ya Maji ya Maziwa Makuu**

35. Katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya majisafi, salama na ya kutosheleza kwa kutumia maziwa makuu, Serikali itaanza ujenzi wa mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika Mkoa wa Simiyu utakaotumia maji ya Ziwa Victoria. Aidha, Serikali itaendelea kuongeza chanzo cha Butimba ili kiweze kuhudumia maeneo mengi zaidi ya Jiji la Mwanza.

**5.2.6 Miradi ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini**

36. Katika kuhakikisha malengo ya Kisekta ya kuwapatia wananchi wa mijini huduma ya maji ya kutosha, Serikali itatumia vyanzo vya uhakika vikiwemo maziwa makuu, mito mikubwa na mabwawa. Wizara imepanga kutekeleza jumla ya miradi 175 ya maji mijini.

37. Serikali inatarajia kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma kupeleka Manispaa ya Mtwara – Mikindani pamoja na vijiji na vitongoji vilivyopo ndani ya kilomita 12 ya bomba kuu; mradi wa kutoa maji mto Kiwira kupeleka Jiji la Mbeya; mradi wa kutoa maji mto Rufiji kupeleka Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya Pwani. Utekelezaji wa miradi hiyo utasaidia upatikanaji wa maji ya uhakika na ya kutosheleza kwa maeneo ya mijini.

**5.2.7 Mpango wa Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Jiji la Dodoma**

38. Serikali inatambua changamoto ya huduma ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wa Jiji la Dodoma kutokana na ongezeko kubwa la watu baada ya makao makuu ya Serikali kuhamia Dodoma na ongezeko la shughuli za kiuchumi na kijamii. Mahitaji ya majisafi katika Jiji la Dodoma kwa sasa yanakadiriwa kuwa ni lita milioni 133.8 kwa siku ambapo uzalishaji katika vyanzo vyote vya maji ni lita milioni 66.7 kwa siku. Hivyo kuna upungufu wa maji katika jiji la Dodoma wa takribani lita milioni 67.1 kwa siku sawa na asilimia 50.2.

39. Katika jitihada za kutatua changamoto hiyo, Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepata mkopo wa Dola za Marekani milioni 125.3 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Bwawa la Farkwa na mtambo wa kusafisha na kutibu maji ambapo ujenzi wake utaanza mwaka wa fedha 2022/23.

40. Katika kutatua changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Dodoma, Serikali inatarajia kutoa maji Ziwa Victoria na kuyafikisha katika Jiji la Dodoma kupitia mji wa Singida. Serikali inaendelea kutafuta fedha vyanzo mbalimbali ili mradi huo uweze kutekelezwa.

**5.2.8 Mpango wa Kuimarisha Huduma ya Uondoshaji Majitaka**

41. Wizara imepanga kuendelea kuboresha huduma ya usafi wa mazingira nchini. Miradi itakayotekelezwa ni pamoja na miradi ya usafi wa mazingira katika miji mikuu 10 ya Vwawa, Kigoma, Lindi, Sumbawanga, Singida, Njombe, Mtwara, Katavi, Tabora na Geita na miji midogo 15 ya Chalinze, Kisarawe, Bagamoyo, Kibaigwa, Igunga, Nzega, Chato, Muleba, Bunda, Mafinga, Ilula, Makambako, Korogwe, Manyoni na Rujewa. Aidha, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi ya usafi wa mazingira katika miji ya Babati, Dodoma, Mbeya, Iringa na Dar es Salaam.

42. Katika kukifanya Chuo cha Maji kuwa bora zaidi na kuweza kutoa wataalam wa maji watakaotumika katika usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji hususan ya vijijini pamoja na kufanya tafiti za kutatua changamoto mbalimbali katika Sekta ya Maji, Serikali imepanga kujenga na kukarabati majengo na miundombinu katika kampasi za Dar es Salaam na Singida; na kununua magari mawili ya uondoshaji majitaka na mafunzo katika fani ya uhandisi wa majitaka. Vile vile wizara itanunua basi kubwa la abiria 65 kwa ajili matumizi ya wanafunzi kuwapeleka katika mafunzo ya vitendo, magari mawili na gari moja kwa ajili shughuli za uendeshaji na usimamizi wa Ofisi za Tawi la Chuo Singida. Pia, serikali imepanga kuboresha kuboresha kituo cha utafiti wa ubora wa maji cha Ngurdoto-Arusha (Ngurdoto Defluoridation Centre).

**6.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/2023**

43. Ninaomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi bilioni mia saba na tisa milioni mia tatu sitini na moja mia sita na saba elfu (709,361,607,000) kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2022/23. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni Shilingi bilioni hamsini na moja milioni mia nne sitini na mbili mia mbili sitini na tisa elfu (51,462,269,000) ambapo Shilingi bilioni kumi na sita milioni mia saba mia tano thelathini na nne elfu (16,700,534,000) ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi bilioni thelathini na nne milioni mia saba sitini na moja mia saba thelathini na tano elfu (34,761,735,000) ni kwa ajili ya kulipa mishahara (PE) ya watumishi wa Wizara, RUWASA na Chuo cha Maji. Jumla ya bajeti ya maendeleo ni Shilingi bilioni mia sita hamsini na saba milioni mia nane tisini na tisa mia tatu thelathini na nane elfu (657,899,338,000) ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni mia nne na saba milioni sitini na nne mia nane na sitini elfu (407,064,860,000) ni fedha za ndani na Shilingi bilioni mia mbili hamsini milioni mia nane thelathini na nne mia nne sabini na nane elfu (250,834,478,000) ni fedha za nje.

# Shahidi adai nyumba ni mali ya baba yake

**Na Grace Gurisha**

SHAHIDI wa kwanza katika kesi ya kughushi makubaliano ya kumiliki nyumba, Twaha Muze amedai katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwamba mkataba wa kiwanja kilichoko Mbezi Luis Dar es Salaam, ni mali ya baba yake mzazi ingawa imeandikwa jina lake.

Twaha alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu wa mahakama hiyo, Romuli Mbuya wakati akitoa utetezi wake baada ya kuulizwa swali na Wakili wa Serikali, Adolf Verandumi.

Alidai sababu ya kuandikwa jina lake katika mkataba huo ni baada ya kupewa fedha na baba yake mzazi kwenda kununua kiwanja hicho wakati baba huyo akiwa safarini kikazi Chalinze mkoani Pwani.

Twaha alidai kuwa yeye ndiye aliyefanya malipo ya hicho kiwanja kwa jina lake baada ya kupewa maelekezo na baba yake mzazi.

Shahidi huyo pia alikiri kufunga ndoa ya serikali mwaka 2017 na Maimuna ambapo walibahatika kupata watoto wawili na mali ambayo amechuma na aliyekuwa mkewe ni viwanja viwili pamoja na kuchimba kisima cha maji katika eneo la baba yake mzazi.

Alidai hakuwahi kujenga nyumba wakati akiwa na mkewe bali walikuwa wanaishi katika nyumba ambayo walipewa na baba yake mzazi kuishi kwa muda wakati huo baba yake alikuwa anafanya kazi Wizara ya Viwanda na Biashara.

Twaha alidai wakati wanakabidhiwa nyumba na baba yake alikuwepo mkewe lakini aliyesaini ni yeye peke yake kwa sababu mkewe wakati huo alikuwa ana hali mbaya kwasababu alikuwa mjamzito ndio maana katika makabidhiano hakuweka sahihi.

Shahidi wa pili katika kesi hiyo ambaye mshtakiwa wa pili Samson Muze, alidai mwaka 2007 alinunua viwanja viwili kutoka kwa Colman Kimaro.

Akiongozwa na Wakili wa Utetezi Alexander Mzikila, shahidi huyo alidai fedha za kununua viwanja hivyo ni baada ya kuwa na fedha wakati anafanya kazi Wizara ya Viwanda na Biashara.

Alidai nyumba hiyo alimkabidhi mtoto wake wa kiume Tuwaha kwa makubaliano ya kuishi kwa muda na aliyekuwa mkewe.

Inadaiwa washtakiwa hao walighushi makubaliano Novemba 9, mwaka 2011 kwamba Samson Muze ni mmiliki wa nyumba ya ghorofa iliyoko Mbezi Luis na kupewa mwanawe wa kiume Tuwaha Muze kuishi kwa muda katika nyumba hiyo.

Pia inadaiwa mwaka 2017, mshtakiwa wa kwanza Tuwaha aliwasilisha nyaraka ya uongo katika kesi ya ndoa namba 66 mwaka 2017 inayomhusu Maimuna Suka na Tuwaha Muze, iliyokuwa Mahakama ya Wilaya ya Kinondoni.

Baada ya kudai hayo, kesi hiyo iliahirishwa hadi Mei 16, mwaka huu kuendelea na utetezi wa mshitakiwa huyo na washtakiwa wako nje kwa dhamana.

Kwa mujibu wa hati mashtaka inadaiwa kati ya Novemba mwaka 2011 na Desemba mwaka 2017 kwa njia ya udanganyifu walighushi makubaliano ya Novemba 9, mwaka 2011 kwamba Samson Muze ni mmiliki wa nyumba iliyoko Mbezi Luis.

Katika shtaka la pili linalomkabili inadaiwa mwaka 2017 mshtakiwa wa kwanza Twaha Muze aliwasilisha nyaraka hizo za uongo katika kesi ya ndoa namba 66/2017 katika Mahakama ya Wilaya ya Kinondoni.

# Mbunge atoa angalizo ujenzi viwanda nchini

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MBUNGE wa Vwawa mkoani Songwe, Japhet Hasunga, ameitaka serikali kutafakari sababu za kufa kwa viwanda vilivyoanzishwa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere wakati ikijipanga kujenga viwanda vipya nchini.

Amesema hatua hiyo itasaidia kuepuka kurudia makosa yaliyosababisha kufa kwa viwanda vingi vilivyoanzishwa na Mwalimu Nyerere.

Akizungumza juzi bungeni jijini hapa juzi, Hasunga aliipongeza Wizara ya Viwanda, Biashara na Mazingira na Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa taarifa yao waliofanya uchambuzi wa kina.

Alisema katika taarifa zote zinaonyesha kwamba ukuaji wa sekta ya viwanda Tanzania umefika asilimia 8.9 na kueleza kuwa katika mazingira yaliyoko ukuaji huo bado upo chini na hauendani na matatizo yaliyoko.

"Huko nyuma nchi yetu ilibahatika kujenga viwanda vya aina zote, toka tumepata uhuru tulijenga karibu viwanda vya aina zote. Tulikuwa na viwanda na ni sera ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na ni moja ya malengo kwamba lazima tujenge viwanda.

"Na viwanda ukiangalia ndiyo vinatoa suluhu ya matatizo yote tuliyonayo, huko nyuma tulikuwa na viwanda vya kuongeza thamani ya mazao, Baba wa Taifa alijenga karibu vyote tulikuwa navyo," alisema.

Hasunga alisema kulikuwa na viwanda vya kuchakata nyama, kuongeza thamani, vya ngozi, vya misitu na mbao.

"Mpaka 1975 viwanda vilikuwapo, vya nguo vilikuwapo, vya korosho vilikuwapo, vya mafuta vilikuwapo, mabati, misumari vilikuwapo, hatukukosa chochote, suala la kujiuliza ni nini kilitokea viwanda vyote vikafa?

"Tukijua pale tulifeli nini ndipo tutakuwa na mkakati unaofaa katika kujenga viwanda kwa sasa. Bila kujua tulikotoka hatuwezi kujenga viwanda," alitahadharisha.

Hasunga aliiomba wizara isaidie kujua upi mkakati wa kuongeza viwanda na ajira Tanzania ambao Bunge likiuangalia litaridhika kwamba nchi itatoka ilipo na kufika wanakotaka iende.

"Pili, upi mkakati wa wizara wa kuongeza tija na thamani ya bidhaa zetu? Bidhaa zetu zipo duni, haziwezi kuhimili ushindani katika soko la dunia, mkakati tulioweka ni upi ili tupate bidhaa zitakazoshindana soko la dunia?


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

## UWASILISHAJI WA TAARIFA ZA WAMILIKI MANUFAA WA MAKAMPUNI

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) inawakumbusha wamiliki wa makampuni yaliyosajiliwa hapa chini kuwa tarehe 30 Juni, 2022 ni siku ya mwisho ya kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa. Taarifa hizo zinatakiwa kuwasilishwa kupitia tovuti ya BRELA (**bo.brela.go.tz**)

Serikali kupitia Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara mnamo mwezi Januari mwaka 2022, iliongeza muda wa miezi sita (6), ya uwasilishaji wa taarifa hizi ili kuwawezesha wamiliki wa makampuni kuteleza kwa ukamilifu takwa hilo la kisheria.

Uwasilishaji wa taarifa za Mmiliki Manufaa una lengo la kuboresha mazingira ya uwekezaji, kuzuia rushwa na utakatishaji fedha, kuongeza utekelezaji wa sheria, kujenga uaminifu na uwajibikaji na hatimaye kuongeza pato la Taifa.

Kwa taarifa hii BRELA inawataka wamiliki wa makampuni ambao bado hawajawasilisha taarifa zao kufanya hivyo katika siku zilizosalia ili kuepuka usumbufu usio wa lazima.

Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana nasi kwa **simu Na: +255 (0) 222 212 800** au barua pepe **usajili@brela.go.tz,** mitandao ya kijamii: Instagram na Twiiter brela_tanzania, Face book: BRELA Tanzania au tembelea tovuti ya BRELA: **www.brela.go.tz**

**Imetolewa na;**
**Kitengo cha Habari na Mawasiliano**

# SHIDA YETU NI POINTI SIYO MABAO -MGUNDA

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda amesema anachohitaji kwa sasa ni ushindi tu na si idadi ya magoli, ili kutoka kwenye eneo la hatari na kupanda juu ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema hayo juzi mara baada ya kumalizika kwa mechi ya Ligi Kuu kati ya timu hiyo dhidi ya Biashara United, ikishinda bao 1-0 nyumbani, Uwanja wa Mkwakwani, Tanga.

Mgunda amesema kuwa wamekuwa wakipambana kwa sasa kuitoa Coastal Union shimoni, hivyo wamekuwa wakitumia angalau nafasi moja wanayoipata, huku akiimarisha eneo la ulinzi lisiruhusu bao, kwa sasa kinachohitajika kwa timu yake ni pointi tatu tu.

"Shida ni pointi siyo mabao, kwa hiyo haijalishi tunashinda vipi. Nahitaji bao moja tu ili nipate pointi tatu, kwa sababu hali iliyopo kwa sasa siyo ya kusema ucheze upate mabao mengi, hapana, kinachotakiwa ni ushindi tu," alisema straika huyo wa zamani wa timu hiyo.

Alisema anamshukuru Mungu kupata ushindi huo kwani ligi imekuwa ngumu, lakini ataendekea kujipanga na vijana wake kupata matokeo mazuri na kuiweka timu hiyo sehemu salama.

Coastal imeshinda mechi mbili mfululizo ushindi wa bao 1-0 na kuipatia jumla ya pointi sita, baada ya Jumapili iliyopita kuitwanga Polisi Tanzania bao 1-0 kwenye uwanja huo huo.

Ni ushindi uliowapandisha hadi kwenye nafasi ya 10 ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikifikisha pointi 27, huku ikiiacha Biashara United ikiwa kwenyе nafasi ya 13 na pointi zake 23.



Mwogeleaji wa Klabu ya FK Blue Marlins, Lorita Borega, akichapa maji.

# Gymkhana Arusha yatoa sababu kushindwa Rwanda

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Gymkhana mkoani Arusha, Godluck Molel amesema timu yao ilishindwa kufanya vizuri katika mashindano ya mchezo wa tenisi Afrika Mashariki yaliyofanyika nchini Rwanda mwaka huu kutokana na changamoto ya viwanja waliyokutana nayo, na hivyo Tanzania kuishia kushika nafasi ya tatu.

Akizungumza na gazeti hili jana kutoka mkoani humo Kocha huyo alisema kama si changamoto hiyo anaamini Tanzania ingeshika nafasi ya kwanza.

"Timu yetu ya Tanzania imeshika nafasi ya tatu katika mashindano hayo kutokana na viwanja tulivyokutana navyo vilikuwa vya vumbi wachezaji wetu hawajavizoea na imechukua muda mrefu kuwajenga kisaikolojia ili waendelee na mashindano," alisema Molel.

Alisema mashindano hayo ambayo yalishirikisha nchi sita yalikuwa na ushindani mkubwa na ilikuwa inahitaji kuipeperusha bendera ya nchi yake.

Kocha huyo alisema anaomba serikali pamoja na Taasisi mbalimbali ziwasaidie kuwaunga mkono ili wafike mbali kupitia mchezo huo.

"Tunaomba serikali itusaidie kutushika mkono ili tutimize mikakati yetu, kwani kuna wakati tunashindwa kuisafirisha timu kwenda kushiriki mashindano nje ya nchi kutokana na ukata wa fedha hadi kushindwa kununua vifaa vya michezo," alisema.

Mashindano hayo yalishirikisha nchi ya Uganda, wenyeji wa mashindano Rwanda, Kenya, Tanzania, Burundi pamoja na nchi ya Comoro.

## Klabu 15 kushiriki mashindano ya FK Blue Marlins

**Na Mwandishi wetu**

KLABU 15 zitashiriki katika mashindano ya kwanza ya kuogelea ya FK Blue Marlins yaliyopangwa kuanza leo kwenye bwawa la kuogelea la shule ya kimataifa ya FK ya Bahari Beach.

Klabu hizo ni Dar Swiming Club, Mwanza Swim Club, Bluefins, Taliss-IST, Lake Swim Club, Champion Rise Club na Arusha Swim Club.

Klabu nyingine ni Wahoo Zanzibar, MIS Piranhas, Braeburn Sharks, Pigec Swim Club, Train 2 Gain Club, Milestone Swim Club, St Constantine International na wenyeji FK Blue Marlins.

Meneja wa klabu ya FK Blue Marlins, Opalina Nanyaro amesema jumla ya waogeleaji 233 watashindana katika mashindano hayo ambayo yatamalizika Jumapili.

Opalina alisema kuwa zawadi mbalimbali zitatolewa kwa washindi katika mashindano hayo yaliyodhaminiwa na Shoppers Kahawa Cafe, Cool Blue, EFM, Doctors Plaza Polyclinic, PRO Fixers Tanzania, FK International Schools, Viscar Integrated Consulting (TZ) Limited na Coca Cola, GardaWorld.

Kwa mujibu wa Opalina waogeleaji watashindana katika umri tofauti katika staili mbalimbali.

Alisema kuwa pia kutakuwa na mashindano ya waogeaji ya watu wakubwa wenye umri kuanzia miaka 25 na kuendelea au Masters.

## Zanzibar yapangwa kundi B kuogelea Uganda

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

ZANZIBAR imepangwa kundi B katika Michuano ya Afrika Mashariki na Kati "CECAFA Women's senior Challenge" inayotarajiwa kuanza kutimua vumbi Mei 22 mwaka huu nchini Uganda.

Katika kundi hilo B Zanzibar itakutana na Tanzania, Sudan Kusini pamoja na Ethiopia.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Wanawake Zanzibar, Abdulmutik Ali Haji alisema hadi sasa wanaendelea na mazoezi ya kujiandaa na michuano hiyo.

Alisema ameona makundi yaliyopangwa hivyo na yeye anajiandaa timu kuweza kushindana na ana matarajio yake kufanya vizuri.

"Nimeona makundi yamepangwa na kundi tulilopangwa ni zuri, kwani kila timu inataka kuiwakilisha vizuri nchi yake na sisi tunaendelea na maandalizi ya kuelekea michuano hiyo," alisema.

Hata hivyo, alisema kuwa wanatarajia kucheza mchezo mmoja wa kirafiki dhidi ya timu ya vijana ya wanaume ili kuangalia sehemu yenye mapungufu na kufanyiwa kazi.

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

### JUVE NA POGBA
JUVENTUS wako tayari kumpa kiungo wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba pauni milioni 8 kwa mwaka pamoja nà marupurupu na ada ya kukubali kutua Juve. Mkataba wa Pogba unamalizika mwishoni mwa msimu huu na Manchester City wanatajwa kumtaka nyota huyo mwenye umri wa miaka 29. ***(Mirror)***

### DEST ATAKIWA CHELSEA
CHELSEA wanamtaka mlinzi wa Barcelona na Marekani, Sergino Dest mwenye umri wa miaka 21. ***(Sport)***

### JESUS KUTUA ARSENAL
WAKALA wa mshambuliaji wa Brazil na Manchester City, Gabriel Jesus ameeleza kwamba nyota huyo mwenye umri wa miaka 25 amefanya mazungumzo na Arsenal kuhusu uwezekano wa kuhamia huko. ***(Guardian)***

### MAN MAMBO MAGUMU
MIPANGO ya usajili wa Manchester United katika dirisha lijalo imeingia mchanga baada ya viungo watatu inaowataka kukataa kwenda Old Trafford. ***(Star)***

### RICHARLISON AIVUTIA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur inavutiwa na wachezaji watatu wa Everton, akiwamo mshambuliaji Mbrazil Richarlison mwenye umri wa miaka 25 winga wa England, Anthony Gordon mwenye umri wa miaka 21 na mlinzi mwenye miaka 24, Ben Godfrey. ***(Telegraph)***

### TIELEMANS AWANIWA SPURS
TOTTENHAM Hotspur pia wanamfuatilia kiungo wa Leicester City na Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 25. ***(GiveMeSport)***

### BERBATOV ATOA ONYO
DIMITAR Berbatov ameiambia klabu yake ya zamani ya Tottenham Hotspur wasijielekeze tu katika kumbakiza nahodha wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 28, msimu huu, kwa sababu klabu kubwa zitamtupia macho pia mshambuliaji wa Korea Kusini, Son Heung-min Heung mwenye umri wa miaka 29. ***(London Evening Standard)***

### OSIMHEN PAUNI MIL. 85
KLABU ya Manchester United imefahamishwa itapaswa kulipa kitita cha pauni milioni 85.5 kama itataka kumsajili mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 23, kutoka Napoli msimu huu. ***(Calciomercato, via Four Four Two)***

### RICE KUBAKIZWA
WEST Ham imempa kiungo wa England, Declan Rice, ambaye anasakwa na klabu za Chelsea na Manchester United, mkataba wa miaka nane atakaolipwa mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki ili abakie klabuni hapo. ***(Talksport)***

### PALHINHA KUMRITHI MOUTINHO
KLABU ya Wolves itamsajili kiungo mchezeshaji wa Sporting Lisbon na Ureno, Joao Palhinha mwenye umri wa miaka 26, kama kiungo wake, Joao Moutinho mwenye miaka 35 ataondoka. ***(Jornal de Noticias)***

### COUTINHO KUBAKI VILLA
KLABU ya Aston Villa inakaribia kutangaza uhamisho wa kudumu wa kiungo wa Brazil na Barcelona, Philippe Coutinho mwenye umri wa miaka 29, ambaye anaicheza Villa Park kwa mkopo tangu Januari. ***(Fabrizio Romano)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# JUVENTUS YATOA OFA KWA POGBA

Aahidiwa mshahara mkubwa, kwenda kuziba pengo la Dybala anayeondoka na...

**TURIN, Italia**

JUVENTUS imetoa ofa ya mkataba ambayo wanaamini wanaweza kumsajili tena Paul Pogba, kwa mujibu wa gazeti la Mirror.

Kuondoka kwa Pogba pale Manchester United mwishoni mwa msimu huu kumekuwa kukikisiwa kwa muda mrefu.

Kuwasili kwa kiungo huyo wa kati Mfaransa mwaka 2016 kwa kipindi cha pili pale Old Trafford kulikuja kwa mkataba uliovunja rekodi ya dunia, lakini hajatimiza matarajio ambayo yaliambatana na bei ya pauni milioni 89.

Hivyo kumekuwa na uvumi mkubwa wa kuhusisha Pogba ambaye ni mshindi wa Kombe la Dunia na Ufaransa 2008 kuondoka kwa mashetani wekundu hao na sasa anaweza kurejea Juventus, klabu ambayo alipata umaarufu mkubwa.

Pogba anakaribia kuondoka Man United mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu, na Juve wameripotiwa kutoa ofa ya mshahara wa pauni milioni 8 kwa mwaka.

Huku kuondoka kwa Paulo Dybala na Giorgio Chiellini kukiwa na nafasi ya ziada ya mshahara, ofa ya Pogba pia inasemekana kujumuisha ada kubwa ya kumsajili na kifurushi cha bonasi ili kukamilisha mpango huo. Pogba mwenye umri wa miaka 29 amekosa mechi nne zilizopita za Mashetani Wekundu za Ligi Kuu England kutokana na matatizo ya mguu, na hakuwapo kwa miezi miwili mapema msimu huu kutokana na jeraha la misuli ya paja.

Mapema wiki iliyopita, Pogba alikuwa akihusishwa na majirani zao Manchester City kabla ya yeye mwenyewe kujitokeza hadharani na kukanusha taarifa hizo.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,255
MECHI KALI
NAMUNGO
VERSUS
MBEYA KWANZA FC
1 | 2.05
X | 2.82
2 | 3.89
PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# DE BRUYNE ALITAKA AFUNGE MATANO



**MANCHESTER, England**

KEVIN De Bruyne alisifu uwezo wake wa kufunga mabao manne kuwa "maalum" baada ya Manchester City kurejesha uongozi wao wa pointi tatu kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu kwa kuwalaza Wolves 5-1, lakini alisema alipaswa kufunga zaidi.

Baada ya kuona Liverpool ikiichapa Aston Villa 2-1 Jumanne, City walitoa kichapo kikali katika uwanja wa Molineux, Jumatano huku De Bruyne akifunga mabao manne, matatu ya kwanza dani ya dakika ya 24 na kuisaidia timu hiyo ya kocha, Pep Guardiola kubakiwa na pointi nne ili kutwaa ubingwa wa ligi hiyo.

Mabao matatu ya awali ya De Bruyne yalimfanya kuwa mchezaji wa tatu kufunga 'hat-trick' ya haraka zaidi ya mwanzo wa mchezo Ligi Kuu, baada ya Sadio Mane kufunga ndani ya dakika 16 dhidi ya Aston Villa, Mei 2015 na Dwight Yorke ndani ya dakika ya 22 dhidi ya Arsenal, Februari 2001.

Mbelgiji huyo aliongeza la nne baada ya saa moja, na kuwa mchezaji wa pili wa City kufunga mabao manne katika mchezo wa ugenini wa Ligi Kuu ya England baada ya Edin Dzeko dhidi ya Tottenham Agosti 2011.

De Bruyne, ambaye anafurahia msimu wake wa ufungaji bora akiwa na City baada ya kufikisha mabao 19 katika michuano yote, alifurahishwa na kiwango chake, lakini alisisitiza kwamba alipaswa kuongeza la tano wakati alipogonga mwamba dakika za mwisho.

"(Ilikuwa) nzuri sana! Unapofunga mabao manne huwa ni kitu maalum, ilipaswa kuwa matano," alisema akiiambia Sky Sports.

"Nadhani tulicheza vizuri, labda isipokuwa mashambulizi kadhaa ya kushtukiza katika kipindi cha kwanza, nadhani tulidhibiti mchezo vizuri.

"Hata tungeweza kufunga zaidi, na kufanya hivyo dhidi ya timu ya Wolves ambayo ina ulinzi mkali.

"Mguu wangu wa kulia ni mguu wangu wenye nguvu zaidi, lakini siogopi kupiga na kushoto."

# Mount: Chelsea ilihitaji ushindi

**LONDON, England**

MASON Mount alibainisha kwamba, Chelsea ilihitaji kurudi kwenye ubora wake katika chumba cha kubadilishia nguo baada ya ushindi wa 3-0 dhidi ya Leeds United, Jumatano kwenye mchezo wa Ligi Kuu England.

Wakitoka katika mechi tatu za Ligi Kuu England bila ushindi, wakidondosha pointi kwa Manchester United, Everton na Wolves, Chelsea walijibu kwa nguvu na kuanza kwa kasi.

Mount alikuwa miongoni mwa wafungaji wa The Blues hao, akifunga bao la kwanza dakika ya nne, kabla ya Christian Pulisic na Romelu Lukaku kuongeza mabao ya kipindi cha pili dhidi ya wenyeji waliomaliza wakiwa 10 dimbani.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 alifichua jinsi walivyoanza kwa nguvu pale kwenye dimba la Elland Road na ilivyokuwa muhimu kwao kupata ushindi kuelekea kwenye fainali ya kombe la FA dhidi ya Liverpool, Jumamosi.



"Tulizungumza kuhusu jinsi wiki hii ilivyokuwa kubwa mwanzoni - haikuanza vyema Jumamosi iliyopita," alisema Mount akiiambia Sky Sports.

"Tulihitaji kurudi kwa nguvu. Tulikuwa na siku chache za kukusanyika na kuzungumza ndani ya kikundi, ukweli fulani ambao ulihitaji kusemwa na tukaiondoa kwenye mfumo wetu.

"Huu ulikuwa mchezo ambao tunaweza kwenda, tunajua nini kitakachofuata. Ni mchezo mkubwa, mkubwa na hii ni hatua nzuri kuelekea hilo."

Mount alifunga kwenye mechi mbili tu za Ligi Kuu kwa mwaka 2022 kabla ya Jumatano, moja ikiwa dhidi ya Norwich, Machi na dhidi ya Southampton, Aprili.

5,316,060

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 14/05/22 | 20:00 | Niort vs Valenciennes | 2.42 | 3.18 | 2.83 |
| 02. 14/05/22 | 20:00 | Nancy vs PAU FC | 2.34 | 3.27 | 2.88 |
| 03. 14/05/22 | 20:00 | Nimes vs Bastia | 2.57 | 3.16 | 2.67 |
| 04. 14/05/22 | 22:00 | Bordeaux vs Lorient | 2.29 | 3.49 | 2.84 |
| 05. 14/05/22 | 22:00 | Toronto FC vs Orlando City | 2.45 | 3.44 | 2.78 |
| 06. 14/05/22 | 22:30 | Colorado Rapids vs Los Angeles FC | 2.39 | 3.57 | 2.77 |
| 07. 15/05/22 | 13:30 | Bologna vs Sassuolo | 2.58 | 3.47 | 2.48 |
| 08. 15/05/22 | 16:00 | Leeds vs Brighton | 2.34 | 3.33 | 2.83 |
| 09. 15/05/22 | 16:00 | Watford vs Leicester | 2.77 | 3.52 | 2.30 |
| 10. 15/05/22 | 16:30 | St. Pauli vs Fortuna Dusseldorf | 2.28 | 3.56 | 2.77 |
| 11. 15/05/22 | 16:30 | Sandhausen vs Holstein Kiel | 2.62 | 3.47 | 2.44 |
| 12. 15/05/22 | 18:30 | Degerfors vs Helsingborg | 2.44 | 3.22 | 2.63 |
| 13. 15/05/22 | 19:30 | Villarreal vs Real Sociedad | 2.31 | 3.56 | 2.80 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 13/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2754 | Slagelse BI vs KFUM Roskilde | 2.34 | 3.63 | 2.52 |
| 14:00 | 3418 | Fremad Amager vs HB Koge | 2.14 | 3.26 | 3.07 |
| 14:00 | 4502 | Greve vs Bronshoj BK | 1.51 | 4.29 | 4.87 |
| 16:00 | 5123 | Namungo vs Mbeya Kwanza FC | 2.05 | 2.82 | 3.89 |
| 17:00 | 5518 | NK Jarun Zagreb vs Rudes Zagreb | 3.21 | 3.21 | 2.10 |
| 17:30 | 5998 | Porto B vs Benfica Lisbon B | 2.31 | 3.51 | 2.72 |
| 18:00 | 1952 | Viktoria Otrokovice vs Vratimov | 1.73 | 3.90 | 3.75 |
| 18:00 | 2696 | Komarno vs FC Petrzalka 1898 | 1.55 | 3.90 | 5.06 |
| 18:00 | 3537 | FC Stk 1914 Samorin vs MFK Dubnica | 1.49 | 4.19 | 5.26 |
| 18:00 | 3705 | AC Oulu vs Honka | 4.76 | 3.60 | 1.63 |
| 18:00 | 4592 | VPS Vaasa vs Seinajoen JK | 2.81 | 3.15 | 2.34 |
| 18:30 | 4849 | Japs vs EIF Ekenas | 3.21 | 3.65 | 1.94 |
| 19:00 | 1099 | Skra Czestochowa vs Puszcza Niepolomice | 2.96 | 3.15 | 2.25 |
| 19:00 | 1159 | Hrvatski Dragovoljac vs HNK Gorica | 4.67 | 3.75 | 1.62 |
| 19:00 | 2789 | Sochi vs Nizhny Novgorod | 1.44 | 4.26 | 6.73 |
| 19:30 | 1374 | SKN St Polten vs Wacker Innsbruck | 1.62 | 4.16 | 4.16 |
| 19:30 | 1970 | SV Lafnitz vs Floridsdorfer AC | 2.77 | 3.25 | 2.32 |
| 19:30 | 2346 | SV Horn vs Austria Lustenau | 4.08 | 3.89 | 1.67 |
| 19:30 | 2774 | Austria Vienna II vs Rapid Vienna II | 2.21 | 3.49 | 2.77 |
| 19:30 | 4512 | Dornbirn vs Vorwarts Steyr | 2.97 | 3.55 | 2.07 |
| 19:30 | 5450 | Blau Weiss Linz vs FC Liefering | 1.71 | 3.79 | 3.98 |
| 19:30 | 5894 | FC Juniors OO vs Kapfenberg | 2.53 | 3.50 | 2.38 |
| 19:30 | 5933 | Amstetten vs Liebherr Gak | 2.06 | 3.60 | 2.97 |
| 20:00 | 2062 | Inter Zapresic vs Bsk Bijelo Brdo | 1.91 | 3.36 | 3.60 |
| 20:00 | 3178 | Dalkurd FF vs Skovde Aik | 2.72 | 3.38 | 2.52 |
| 20:00 | 3454 | Hlucin vs Velke Mezirici | 1.38 | 5.60 | 6.00 |
| 20:00 | 4602 | Viseu vs Penafiel | 2.44 | 3.41 | 2.62 |
| 20:30 | 2536 | Friska Viljor FC vs IF Algarna | 1.55 | 4.40 | 5.20 |
| 21:30 | 2146 | Jagiellonia vs Legia Warszawa | 3.02 | 3.21 | 2.19 |
| 21:30 | 2251 | Podbeskidzie Bie vs Arka Gdynia | 2.25 | 3.31 | 2.83 |
| 21:45 | 1047 | Shelbourne vs Drogheda Utd | 2.04 | 3.11 | 3.45 |
| 21:45 | 1214 | Annecy FC vs Sedan | 1.39 | 4.42 | 7.27 |
| 21:45 | 1359 | Cholet vs Chateauroux | 3.53 | 3.39 | 1.97 |
| 21:45 | 1362 | Shamrock Rovers vs Derry City | 1.76 | 3.41 | 4.19 |
| 21:45 | 1635 | Villefranche Sur Saone vs Bourg Peronnas | 1.57 | 3.93 | 5.12 |
| 21:45 | 1767 | Chambly vs Boulogne | 2.46 | 3.10 | 2.81 |
| 21:45 | 3348 | Treaty United vs Bray Wanderers | 2.26 | 3.22 | 2.88 |
| 21:45 | 4023 | Avranches vs Creteil | 2.42 | 3.24 | 2.75 |
| 21:45 | 4031 | Luton Town vs Huddersfield | 2.33 | 3.02 | 3.12 |
| 21:45 | 4656 | Bastia Borgo vs Sete 34 FC | 2.10 | 3.21 | 3.36 |
| 21:45 | 4720 | Arbroath vs Inverness | 2.41 | 3.13 | 2.94 |
| 21:45 | 5135 | Waterford Utd vs Cobh Ramblers | 1.28 | 5.07 | 8.38 |
| 21:45 | 5441 | Wexford Youths vs Galway United | 3.46 | 3.41 | 1.93 |
| 21:45 | 5445 | Athlone Town vs Longford Town | 4.56 | 4.08 | 1.57 |
| 21:45 | 5682 | Dundalk FC vs Bohemians FC | 2.00 | 3.41 | 3.26 |
| 21:45 | 5729 | Orleans vs Laval | 2.95 | 3.19 | 2.31 |
| 21:45 | 5873 | Red Star vs Concarneau | 2.77 | 3.16 | 2.45 |
| 22:00 | 1692 | Finn Harps vs UCD Dublin | 1.58 | 3.69 | 5.05 |
| 22:00 | 4484 | Real Sociedad B vs Almeria | 3.76 | 3.51 | 1.89 |
| 22:15 | 5282 | Pacos Ferreira vs Benfica | 6.59 | 4.80 | 1.40 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# WADAU WAOMBWA KUJITOKEZA KUDHAMINI MUZIKI WA DANSI

**Na Sabato Kasika**

MASHABIKI wa muziki wa dansi nchini, wameombwa kujitokeza kwa wingi kudhamini maonyesho ya muziki huo, kama njia mojawapo ya kuuwezesha kurudi kwenye chati kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Hatua hiyo inatokana na kile kinachoelezwa kuwa, kwa muda mrefu muziki wa dansi umeendelea kudorora huku kukiwa na juhudi ndogo za kuuwezesha kupata nguvu, hali ambayo inawezekana ukafa.

Wito huo ulitolewa jijini Dar es Salaama juzi, na Ofisa Uhusiano wa Mo Green International Kessa Mwambeleko alipokuwa akizungumzia onyesho la 'Wafia Dansi' linalotarajiwa kufanyika Dar es Salaam Mei 28 mwaka huu.

Onyesho hilo litashirikisha bendi tano za Msondo Ngoma Music, Bogoss Music, Mapacha Music zote za Dar es Salaam, Mjengoni Classic ya Arusha na Waluguru Orignal ya Morogoro.

Kessa alisema, kampuni yake imedhamini onyesho hilo ambalo lengo lake ni kufufua muziki huo nchini, na kwamba juhudi hizo zinapaswa kuungwa mkono na wadau wengine ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

"Wito wangu kwa wadau wengine wa dansi wajitokeze kwa wingi kuungana nasi kudhamini muziki huo ili kusaidia kuurudisha kwenye chati kama ilivyokuwa miaka ya nyuma," alisema Kessa.

Kessa alifafanua kuwa Mo Green International inajihusisha na uagizaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo nchini, lakini imeamua kudhamini muziki wa dansi ili kuhakikisha unapata nguvu.

Alisema, bendi za dansi zina nyimbo nyingi zenye ujumbe kwa jamii kutokana na tungo na kwamba ndiyo sababu ya kampuni yake kudhamini onyesho la Wafia Dansi kwa miaka miwili mfululizo.

Naye Mratibu wa onyesho hilo la 'Wafia Dansi' kutoka kampuni ya Cheza Kidansi Entertainment Benard James, aliomba Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na Chama cha Muziki wa Dansi Tanzania (CHAMUDATA) kutoa kipaumbele katika bendi za muziki wa dansi ili kufika mbali.

"Ninaamini kwamba, muziki wa dansi una mashabiki wengi, hivyo ni vyema kuuendeleza ili vizazi vijavyo viweze kufahamu nyimbo zenye ujumbe mzuri na maadili ya nchi yetu, " alisema James.



Ofisa Uhusiano wa Mo Green, Kessa Mwambeleko (kulia), akizungumza kuhusu umuhimu wa kudhamini muziki wa dansi. Katikati ni Rais wa bendi ya Mapacha Music, Jose Mara na Mratibu wa onyesho la 'Wafia Dansi', Benard Jamee. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Namungo yaapa kurudi nafasi ya tatu

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Namungo leo kinashuka kwenye uwanja wa nyumbani, Ilulu mjini Lindi kucheza dhidi ya Mbeya Kwanza, huku ikiapa kutaka kurejea kwenye nafasi ya tatu ambayo itaifanya kucheza michuano ya kimataifa msimu ujao.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo Jamhuri Kihwelo 'Julio' amesema tayari ameshaliandaa jeshi lake kwa ajili ya kusaka pointi tatu, ili kurejea tena kwenye nafasi hiyo ambayo wanaitaka kwa udi na uvumba.

"Haitokuwa mechi rahisi, wao wanataka ushindi ili wasishuke daraja na sisi tunataka nafasi hiyo ili kukaiwakilishe nchi kwenye michuano ya kimataifa, itakuwa mechi ngumu sana, lakini tumejiandaa kwa hilo," alisema Julio.

Naye straika wa timu hiyo Jacob Massawe amesema wachezaji wote wa Namungo wamepata mshtuko, kwani baada ya sare ya mabao 2-2 dhidi ya Simba walikuwa kwenye nafasi ya tatu, lakini kwa sasa wameshuka hadi nafasi ya sita kutokana na timu zingine kushinda, hivyo mshtuko huo umewapa morali a kupambana ili kushinda mechi ya leo na kurejea kwenye nafasi yao ya awali.

Iwapo itashinda leo, Namungo yenye pointi 30, itaiengua Azam yenye pointi 32 na kukaa juu yake, lakini nafasi ya tatu wiki hii itategemea na matokeo kati ya Ruvu Shooting dhidi ya Geita Gold, mechi iliyochezwa jana.

Kama Geita Gold yenye pointi 31 ikishinda, itakwea kwenye nafasi ya tatu kwa pointi 34, hivyo hata Namungo ikishinda itakaa kwenye nafasi ya nne.

Mbeya Kwanza ndiyo timu inayoshika mkia kwa sasa ikiwa na pointi 21 kwa michezo 22 ambayo imeshacheza.

# Michezo

Ijumaa Mei 13, 2022
Nipashe



## Juventus yatoa ofa kwa Pogba



Wachezaji wa Yanga kutoka kushoto, Chrispin Ngushi, Saidi Ntibazonkiza, Khalid Aucho na Yusuph Athuma (nyuma), baada ya mazoezi ya kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Dodoma Jiji utakaopigwa Jumapili hii kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Dodoma. **PICHA: YANGA**

# YANGA SC: MALENGO YA UBINGWA YAKO PALEPALE

●●●Yawataka mashabiki wasife moyo, waungane na wasonge mbele kuhakikisha yanatimia na...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imewaondoa shaka wanachama na mashabiki wake kutokana na sare mfululizo ambazo imekuwa ikizipata, ikidai ni hali ya kawaida, ikiwataka wasife moyo, bali waungane katika kipindi hiki ambacho ubingwa upo kwenye mikono yao.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli amesema hayakuwa malengo yao kupata matokeo hayo, lakini ndivyo ilivyotokea na hiyo inaonyesha jinsi ligi ilivyo ngumu.

Jumatatu iliyopita, Yanga illazimishwa suluhu nyumbani dhidi ya Prisons, Uwanja wa Benjamin Mkapa, hali iliyozua taharuki kwa wanachama na mashabiki wao.

"Tunajua matokeo yametuathiri, lakini tunatakiwa tusonge mbele. Ni matokeo ambayo yametupa changamoto na siku zote changamoto ni kipimo cha maarifa ya binadamu, badala ya kulumbana, tunatakiwa tutafute maarifa mapya. Mbio za ubingwa zipo pale pale, tusianze kutoka kwenye reli, tunaongoza ligi na tunatakiwa kushinda tu na si kupiga ramli ya nani ashinde nani apoteze kama wenzetu," alisema Bumbuli.

Alisema kuwa tayari kikosi hicho kimesharejea kambini kujiandaa na mechi dhidi ya Dodoma Jijini itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Jamhuri, Dodoma saa 1:00 usiku.

"Tumerejea kambini, benchi la ufundi limeona makosa yaliyojitokeza, watahakikisha wanafanyia kazi ili yasijirudie tena kwenye mechi dhidi ya Dodoma Jiji," alisema Bumbuli.

Wanachama na mashabiki wa Yanga wamekuwa na sintofahamu baada ya timu yao kutoka suluhu mfululizo kwenye mechi za kuelekea kumaliza msimu wa ligi, huku ikiwa kwenye nafasi nzuri ya kutwaa ubingwa.

Ilitoka suluhu bila kufungana dhidi ya Simba Aprili 30, matokeo kama hayo ikayapata Mei 4 dhidi ya Ruvu Shooting, kabla ya Jumatatu iliyopita, kukutana na matokeo hayo hayo dhidi ya Prisons.

## Pablo atoa siri ya ushindi Kagera Sugar

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Pablo Franco, amefichua siri ya ushindi wao dhidi ya Kagera Sugar kuwa ni kuingia na mbinu tofauti hali ambayo iliwafanya wamepata ushindi wa mapema.

Wakati Pablo akisema hayo Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza amesema Simba iliwazidi ujanja kwa kuziba njia ambazo wangeweza kupata ushindi.

Simba ilifanikiwa kulipa kisasi dhidi yaa Kagera Sugar kwa kuifunga mabao 2-0 katika mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania uliopigwa juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Pablo alisema hakuwa na namna nyingine ya kufanya zaidi ya kubadili mbinu kwa wachezaji wake dhidi ya Kagera na kufunga mabao ya mapema.

"Kipindi cha kwanza tulipata ushindi wa mapema hilo lilikuwa jambo la kwanza na kipindi cha pili niliwaambia kwamba wanapaswa wapate muda wa kupumzika na kucheza kwa umakini," alisema Pablo.

Aliongeza: "Ilikuwa ni ngumu ukizingatia hakukuwa na viungo wa asili kwenye eneo la ukabaji pamoja na wale wa kutengeneza nafasi, ilibidi nije kwa mtindo wa kipekee na tulishinda mchezo wetu," alisema Pablo.

Alisema amelazimika kubadili mbinu hizo kwa sababu ya asilimia kubwa ya viungo wake kuwa majeruhi na wengine kupewa mapumziko mafupi kutokana na kutoka katika matibabu.

Kikosi cha Simba kimerejea kambini jana kwa ajili ya maandalizi ya mchezo wa hatua ya robo fainali ya kombe la Shirikisho dhidi ya Pamba FC, utakaopigwa Jumamosi hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Naye Kocha wa Kagera, Baraza aliwapongeza vijana wake licha ya kukubali kichapo hicho.

"Ukiangalia kipindi cha kwanza tulifanya makosa na Simba wakatumia kufunga mabao ya mapema lakini wamekuwa wajanja sana kwa sababu kipindi cha pili tulicheza vizuri na Simba wamekuwa wajanja na kugoma kuingia katika mtego wetu," alisema Baraza.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042